

**UCHAMBUZI LINGANISHI WA FANI NA MAUDHUI YA NYIMBO ZA  
HARUSI ZA KIMERU NA ZA KISWAHILI**

**NA  
NORAH WANJA GITONGA  
C50/67131/2013**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA  
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA  
NAIROBI.**

**2017**

## **UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na hajatolewa kwa mahitaji ya Shahada katika Chuo kingine chochote.

Sahihi..... Tarehe.....

**Norah Gitonga**

**C57/67131/2013**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi..... Tarehe.....

**PROF RAYYA TIMAMMY**

Sahihi..... Tarehe.....

**PROF. MWENDA MBATIAH**

## **TABARUKU**

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu Bwana na Bibi Luka Njagi, mume wangu Bwana Samuel Gitonga na watoto wangu Sharon, Shillah na Collins.

## **SHUKRANI**

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema maishani mwangu. Ningependa pia kuwashukuru wengi ambao walinifaa kwa hali na mali katika pilkapilka zangu za kuishughulikia kazi hii. Usaidizi wao kwa njia tofauti tofauti ulinifaidi katika kukamilisha kazi hii.

Nawavulia kofia wasimamizi wangu Profesa Rayya Timammy na Profesa Mwenda Mbatiah kwa uvumilivu wao, uelekezi mwema na uongozi wao . Nawashukuru pia wahadhiri wangu waliojitelea mhanga kuniandaa kiusomi hadi kuweza kuikabili kazi hii ya kitaalamu. Baadhi yao ni Dkt. Swaleh, Dkt. Omboga, Dkt. Mweri, Prof. Iribemwangi na Prof. Habwe , aliyekuwa mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili. Weledi na ustadi wao ndio ulionipa hamu ya kutaka kuendelea kusoma hadi nikatunukiwa shahada ya uzamili. Nawashukuru wenzangu ambao tulikuwa pamoja katika safari hii ya kiusomi, wakiwemo Emily Mosota, Simon Kihara, Florence Asiko, Florah Chepkorir,Winnie Kamau,Faith Muchiri na Misheck Nkanga. Mijadala kadhaa tuliyoshiriki ilirahisisha mambo yalipoonekana magumu. Ningependa kuwashukuru wazazi wangu, ndugu zangu na marafiki, ambao walinifaa pakubwa. Wahisani hawa ni wengi ajabu, hivyo basi, nawaomba wapokee shukrani zangu nyingi, na Mungu wa baraka awazidishie mema maishani mwao.

## **IKISIRI**

Tasnifu hii imeshughulikia uchambuzi linganishi wa fani na maudhui katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili. Tumerejelea nadharia mbili, ambazo ni nadharia ya uhalisia na umitindo. Nadharia ya uhalisia imetusaidia katika ufanuzi wa maudhui, nao mtazamo wa umitindo wa Leech (1969) imetusaidia kubainisha vipengele vya fani ambavyo msanii ametumia ili kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Lengo letu ni kulinganisha na kutofautisha maudhui na fani katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili. Tumefanya hivi kwa kukusanya baadhi ya nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili, na hatimaye kuzichambua. Tumezipata nyimbo hizo kwa kufanya utafiti wa nyanjani kwa kuhudhuria sherehe za harusi, kuwahoji watu wenye tajriba katika nyimbo hizo na pia kwa kutumia mitandao. Nadharia tete ambazo tumetumia ni kutaka kuthibitisha iwapo kuna uhusiano na tofauti za kimaudhui na kifani katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili. Utafiti wetu umetuwezesha kuthibitisha kuwa kuna baadhi ya maudhui ambayo yanalingana katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili. Vile vile tumeweza kuthibitisha kuwa kuna fani zinazolingana na pia kutofautiana katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili. Katika kuhitimisha utafiti wetu, tumegusia changamoto tulizokumbana nazo na tukatoa mapendekezo ambayo yanaweza kuwafaa watafiti wa hapo baadaye.

## YALIYOMO

UNGAMO.....	ii
TABARUKU.....	iii
SHUKRANI .....	iv
IKISIRI .....	v
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
1.0 Utangulizi .....	1
1.1 Tatizo la Utafiti.....	2
1.2 Madhumuni ya Utafiti.....	3
1.3 Nadharia Tete .....	3
1.4 Sababu za Kuchagua Mada .....	3
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti .....	5
1.6 Msingi wa Kinadharia.....	6
1.6.1 Mtazamo wa umitindo wa Leech (1969).....	6
1.6.2 Nadharia ya Uhalsia .....	9
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo la Utafiti .....	13
1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nyimbo kwa Jumla .....	13
1.7.2. Yaliyoandikwa Kuhusu Nyimbo za Harusi .....	16
1.8. Mbinu za Utafiti.....	17
1.8.1 Utafiti Maktabani .....	18
1.8.2. Utafiti wa Nyanjani .....	18
1.8.3. Mahojiano .....	18
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>19</b>
2.0 Utangulizi .....	19
2.1 Dhana ya Maudhui.....	19
2.2. Maudhui ya Nyimbo za Harusi za Kimeru .....	21
2.2.1. Kupongeza / Kusifu Maarusi .....	21
2.2.2. Ushauri na Mawaidha kwa Maarusi.....	22
2.2.3. Kufana kwa Harusi.....	25
2.2.4. Kuomba Msamaha .....	26
2.2.5. Kutahadharisha .....	28
2.2.6. Kumkaribisha Bibi Harusi Nyumbani.....	28
2.2.7. Maudhui ya Kukejeli.....	29

2.2.8. Maudhui ya Kuburudisha .....	30
2.7.9. Maudhui ya Maombi / Dua.....	31
2.7.10. Maudhui ya Majukumu ya Maarusi .....	32
2.3. Maudhui ya Nyimbo za Harusi za Kiswahili .....	34
2.3.1 Maudhui ya Maombi / Dua.....	34
2.3.2. Ushauri kwa Maarusi .....	35
2.3.3 Maudhui ya Kuwahimiza Maarusi.....	37
2.3.4 Majukumu ya Maarusi .....	38
2.3.4.1 Makazi Mema .....	38
2.3.4.2 Kushauriana na Kuelekezana.....	38
2.3.4.3 Majukumu ya Nyumbani .....	39
2.3.5. Mapenzi .....	40
2.3.6 Maudhui ya Kuburudisha .....	42
2.3.7. Kufana kwa Harusi.....	43
Hitimisho.....	45
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>46</b>
3.0 Utangulizi .....	46
3.1 Fani katika Nyimbo za Harusi za Kimeru.....	46
3.1.1 Toni .....	46
3.1.1.1 Toni ya Furaha .....	47
3.1.1.2 Toni ya Huzuni .....	47
3.1.1.3 Toni ya kukejeli .....	48
3.1.2 Matumizi ya Tamathali za Usemi .....	48
3.1.2.1 Tamathali za Mafumbo .....	48
3.1.2.2 Tamathali za Mlinganisho .....	49
3.1.2.3 Tamathali za Msisitizo .....	50
3.1.3 Takriri .....	51
3.1.4 Kubadilisha na Kuchanganya Ndimi .....	52
3.1.5 Utohozi .....	52
3.2 Fani katika Nyimbo za Harusi za Kiswahili.....	54
3.2.1 Toni .....	54
3.2.1.1 Toni ya Furaha .....	54
3.2.1.2 Toni ya Unyenyekevu .....	55
3.2.1.3 Toni ya Mapenzi .....	56

3.2.2 Matumizi ya Tamathali za Usemi .....	56
3.2.2.1 Tamathali za Mafumbo .....	56
3.2.2.2 Tamathali za Msisitizo .....	58
3.2.3 Takriri.....	60
3.2.4 Kubadilisha na Kuchanganya Ndimi .....	61
3.2.5 Maswali ya Balagha .....	62
3.2.6 Kufupisha na Kurefusha Maneno. ....	62
Hitimisho.....	63
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>64</b>
4.0 Utangulizi .....	64
4.1. Ulingenishaji wa Maudhui katika Nyimbo za Harusi za Kimeru na Kiswahili ...	64
4.1.1. Maudhui Yanayolingana .....	64
4.1.1.1 Ushauri na Mawaidha kwa Maarusi.....	64
4.1.1.2. Kupongeza au Kusifu Maarusi.....	65
4.1.1.3. Maombi au Dua.....	65
4.1.1.4 Kufana kwa Harusi.....	66
4.1.1.5 Kuburudisha.....	66
4.1.2 Maudhui Yanayotofautiana .....	67
4.1.2.1. Kuomba Msamaha .....	67
4.1.2.2 Mapenzi .....	67
4.1.2.3 Maudhui ya Maombi au Dua .....	67
4.1.2.4. Maudhui ya Mawaidha na Ushauri .....	68
4.2 Ulingenishaji wa fani katika Nyimbo za Harusi za Kimeru na Kiswahili ...	68
4.2.1 Fani Zinazolingana.....	68
4.2.1.1 Toni .....	68
4.2.1.2 Matumizi ya Tamathali za Usemi .....	68
4.2.1.3 Takriri .....	69
4.2.1.4 Kubadilisha na Kuchanganya Ndimi.....	69
4.2.2. Fani Zinazotofautiana.....	69
4.2.2.1 Toni .....	70
4.2.2.2 Tamathali za Usemi.....	70
4.2.2.3 Kuchanganya na Kuhamisha Ndimi.....	70
4.2.2.4 Utohozi .....	71
4.2.2.5. Kufupisha na Kurefusha Maneno.....	71

Hitimisho.....	71
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>72</b>
5.0 Utangulizi .....	72
5.1 Muhtasari wa Utafiti .....	72
5.2 Changamoto katika Utafiti wetu.....	73
5.3 Mapendekezo.....	74
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>75</b>
<b>KIAMBATISHO .....</b>	<b>78</b>

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Utafiti huu unahusu uchambuzi linganishi wa fani na maudhui ya nyimbo za harusi za Wameru na Waswahili. Jamii ya Wameru inapatikana katika kaunti ya Meru, mashariki mwa Kenya. Kaunti ya Meru imegawanyika katika jumuia tatu kuu,nazo ni Tigania, Igembe na Imenti. Eneo la Tigania limegawanyika katika sehemu mbili,nazo ni Tigania Mashariki na Tigania Magharibi.Eneo la Igembe limegawanyika katika sehemu mbili,nazo ni Igembe Kaskazini na Igembe Kusini.Eneo la Imenti limegawanyika katika sehemu tatu kuu ,nazo ni Imenti Kaskazini,Imenti ya kati na Imenti Kusuni.

Jamii ya Waswahili ni pana sana katika pwani ya Kenya, kwa mfano, Waswahili wa Mombasa, Lamu, Unguja, Zanzibar na Kadhalika.Kwa mujibu wa Odeo, na Maina, (2008), Kiswahili ni lugha ambayo ina lahaja nyingi kutegemea maeneo mbalimbali. Hakuna makubaliano kamili kuhusu idadi ya lahaja za Kiswahili na mipaka yake.Hata hivyo, wachunguzi kadhaa wametaja lahaja zifuatazo kwa misingi ya kimaeneo.Waswahili wanaopatikana katika kisiwa cha Unguja yaani Zanzibar mjini na viunga vyake huzungumza lahaja ya Kiunguja. Wale wanaopatikana katika maeneo ya pembeni ya mji wa Mombasa wanazungumza lahaja ya Kijomvu au Chijomvu. Waswahili wanaopatikana katika kisiwa cha Lamu wanazungumza Kiamu. Wale wanaopatikana kwenye maeneo ya Vanga, Tanga, Rufiji, Kilwa, Dar es salaam na Pangani nchini Tanzania wanazungumza Kimrima. Lahaja nyinginezo ni kama vile Kipate, Kisiu, Kimtang'ata, Kivumba na nyinginezo.Utafiti huu unahusu Waswahili wanaopatikana katika kisiwa cha Mombasa wanaozungumza lahaja ya Kimvita.

Fasihi ni kielelezo cha hisia za mwandishi au msimulizi zinazomuathiri akilini, kwenye makazi yake, katika shughuli zake za kila siku, mazingira anamoishi na matukio mbalimbali yanayohusu jamii yake. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), fasihi ni sanaa inayotumia lugha na ambayo hujishughulisha na binadamu pamoja na maisha yake na huathiri, hugusa, au huacha athari fulani na hupatikana katika umbo ambalo linatambuliwa na jamii fulani. Fasihi ni sanaa inayotumia lugha na ina maudhui. Kipera cha nyimbo ni sehemu muhimu sana katika maisha ya binadamu. Nyimbo, hasa za harusi miiongoni mwa aina nyinginezo za nyimbo, hufaidi wanajamii kwa

maudhui teule ambayo hupitishwa kwa nyimbo hizo. Tafiti nyingi za awali zimelenga nyimbo hasa katika somo la fasihi. Ni muhimu kuelewa zaidi nafasi ya nyimbo katika kuendeleza fasihi simulizi ya Kiswahili. Hivyo basi utafiti wetu unahu fani na maudhui ya nyimbo za harusi katika jamii za Wameru na Waswahili.

Kwa mujibu wa Matei (2011), kila jamii ina nyimbo zake ambazo hutofautiana na nyimbo za jamii nyingine. Nyimbo hutambulisha jamii kwa kusawiri shughuli na maisha ya jamii iliyozibuni; kwa mfano, nyimbo za harusi zitasheheni msamati unaodhahirisha mapenzi kati ya maarusi. Vile vile, nyimbo huburudisha na kupitisha ujumbe kwa wanajamii waliozibuni. Anaendelea kusema kuwa nyimbo hupitisha amali na mambo ambayo jamii inayathamini. Amali hizo hurekodiwa katika nyimbo mbalimbali na kurithishwa vizazi vya jamii hiyo. Mawaidha na thamani za jamii hukaririwa katika nyimbo kama nyenko za kuzirithisha. Nyimbo pia hutumiwa kuhamasisha watu na kuchochea hisia za kuchangamkia jambo fulani, kwa mfano, madhara ya ugonjwa fulani, tabia hasi na mengineyo. Nyimbo huakisi ukwasi wa tamaduni za jamii. Umbuji na ujumi wa jamii hujitokeza katika nyimbo.

Katika jamii za Kiafrika, nyimbo hufungamana na muktadha fulani. Kwa mujibu wa Mulokozi (1996), kuna nyimbo za kazi, jando, nyimbo za watoto au bembelezi, vita na kadhalika. Nyimbo hukuza ubunifu mionganoni mwa wanajamii. Uimbaji ni kipawa, na nyimbo hupalilia kipawa hicho.

Utafiti wetu umezingatia uchambuzi linganishi wa fani na maudhui ya nyimbo za harusi katika jamii za Wameru na Waswahili. Tumezingatia jinsi ambavyo maudhui yanalingana na vile vite kutofautiana katika jamii lengwa. Tumechunguza matumizi ya fani mbalimbali katika kuwasilisha ujumbe kwa maarusi, huku tukizingatia kufanana na kutofautiana kwa fani hizo. Tumechunguza sababu zilizomfanya msanii atumie fani fulani, kwa mfano, ili kuficha uso wa maarusi, msanii ametumia lugha yenye mafumbo.

### **1.1 Tatizo la Utafiti**

Wasomi mbalimbali wamefanya utafiti kuhusu fasihi simulizi ya Kiafrika. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), fasihi simulizi ni mali ya jamii, na hakuna mtu binafsi anayeweza kudai kwamba fani hii ni yake. Fasihi simulizi inapitishwa kutoka kwa

kizazi kimoja hadi kingine katika jamii fulani. Utafiti huu unabainisha maudhui ya nyimbo za harusi katika jamii za Wameru na Waswahili, na hatimaye kutathmini jinsi maudhui haya yanavyolingana na kutofautiana. Tumechunguza maudhui katika nyimbo za zamani za harusi katika jamii zote mbili, na vile vile maudhui ya nyimbo zinazoimbwa katika harusi za kisasa na jinsi ambavyo maudhui haya yanavyolingana au kutofautiana, na sababu za mabadiliko hayo.

Swala lingine muhimu tulilosughulikia ni kuhusu fani. Fani ni jumla ya nyenzo zinazotumiwa na msanii ili kuwasilisha maudhui. Tumechunguza fani mbalimbali ambazo wasanii walitumia katika nyimbo hizi za harusi katika nyimbo za hapo awali na zile za kisasa, jinsi ambavyo fani hizi zinalingana na kutofautiana, na jinsi ambavyo tofauti hizi zinachangia katika uwasilishaji wa ujumbe wa msanii.

## **1.2 Madhumuni ya Utafiti**

Lengo kuu la utafiti ni kulinganisha na kutofautisha fani na maudhui ya nyimbo za harusi katika jamii za Wameru na Waswahili kwa :-

- (i) Kuonyesha nyimbo mbalimbali zinazoimbwa katika harusi miongoni mwa jamii za Wameru na Waswahili.
- (ii) Kubainisha maudhui katika nyimbo za harusi za Wameru na Waswahili.
- (iii) Kubainisha aina mbalimbali za fani zilizotumiwa katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii hizi mbili.
- (iv) Kulinganisha na kutofautisha fani na maudhui ya nyimbo za harusi za Wameru na Waswahili.

## **1.3 Nadharia Tete**

Vipera vya fani vilivyotumika katika nyimbo za harusi vimechangia pakubwa katika uwasilishaji wa maudhui.

## **1.4 Sababu za Kuchagua Mada**

Kulingana na Makange (2015), katika tasnifu yake ya uzamili, fasihi simulizi hutumiwa na jamii nyingi za Kiafrika kama njia ya pekee ya kuhifadhi tamaduni zao. Fani zitumiwazo ni pamoja na nyimbo, methali, misemo, ngano, hurafa, ushairi na kadhalika. Fasihi simulizi yaelekeea kupotea miongoni mwa jamii za Kiafrika, kama

vile Wameru na Waswahili, kwa sababu ya mwingiliano mkubwa wa jamii hizi na makabila mbalimbali humu nchini. Baadhi ya wanajamii hawa huzitazama tamaduni zao kama ni duni na hazifai, hivyo basi kuiga tamaduni za Kimagharibi ambazo huziona kuwa ni bora. Isitoshe, kuingizwa kwa mifumo ya maendeleo ya Kimagharibi na maendeleo ya kiutandawazi imezifanya jamii nyingi kupuuza tamaduni zao, hasa wakiziona kama ni mambo ya kishenzi yaliyopitwa na wakati. Hii ndiyo mojawapo ya sababu ya kuamua kufanya utafiti ili kuhifadhi fani na maudhui katika nyimbo za harusi za Wameru, kwani ni kipengele ambacho hakijashughulikiwa kwa kina hapo awali, kinyume na jamii ya Waswahili, ambayo Timammy (2002) amefanya utafiti wake wa fani na maudhui. Uchambuzi linganishi wa fani na maudhui ya nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Wameru na Waswahili ni swala ambalo bado halijashughulikiwa. Pengo hili ndilo lililotupa msukumo wa kuchagua mada yetu.

Nyimbo huelimisha na kufanikisha upataji wa maarifa tofautito fauti kwa wanajamii. Nyimbo pia huwahamasisha watu kutenda mambo fulani au kushirikiana katika matendo tofauti tofauti, hivyo huleta uchangamfu. Kwa hivyo kuna haja ya kutafiti juu ya nyimbo za harusi za jamii ya Wameru na Waswahili, kwani ndoa na familia ni asasi muhimu sana katika jamii.

Kwa kurejelea majukumu yanayoteklezwa na nyimbo katika jamii, ni dhahiri kwamba kwa kubainisha maudhui ya nyimbo za harusi katika kuendeleza fasihi simulizi, tunajaribu kuwashimiza na kuwatolea changamoto wasomi na wahakiki wa Kiswahili kutazama upya dhana ya fani na maudhui. Tunatarajia kwamba utafiti wetu utakuwa wa manufaa kwa wasomi wa Kiswahili.

Inasikitisha kuona kuwa ngoma au nyimbo za kitamaduni zinatoweka, moja kwa moja, na nafasi yake kuchukuliwa na midundo inayozalishwa na tarakilishi. Vijana wetu hawana nguvu za kucheza ngoma ila kuingia katika tarakilishi na kututolea ngoma, na nyimbo zilizojaa vituko chungu nzima. Janga hili limetupa msukumo wa kuchagua mada yetu, kwani fasihi simulizi inalo jukumu la kuuhuisha utamaduni wa Kiafrika. Ni dhahiri kuwa jamii ya kisasa inajaribu kuendeleza fasihi simulizi kwa njia mbalimbali kama vile sherehe za harusi, jando, mazishi na matambiko na njia nyinginezo.

Nyimbo za harusi huwa na umuhimu mkubwa kwa wanajamii, kama vile kuwahimiza na kuwaelekeza maarsi, kuwasifu wanaohusika,kuakisi mtazamo wa jamii kuhusu ndoa na kutaja majukumu ya anayeo na anayeolewa. Nyimbo za harusi pia huonyesha jinsi wanajamii walivyo na fahari kwenye utamaduni wao. Ni jukumu letu sote tunaouheshimu utamaduni wetu kuwashirikisha vijana wetu katika shughuli mbalimbali za kitamaduni,bora tu zisiwe na athari mbovu ili wasitokomee vururu. Utafiti wetu umetusaidia kuhamasisha wanajamii kuhusu fani na maudhui ya nyimbo za harusi katika jamii zilizolengwa. Uimbaji hausaidii tu katika kupidisha ujumbe, bali hata kutimiza lengo la mwimbaji na mtazamaji na pia kufanya shughuli zote za utambaji kufana na kuwa na mguso kwa hadhira.Hii ni mojawapo ya sababu iliyotuvutia kuchagua mada ya fani na maudhui katika nyimbo za harusi za Wameru na za Waswahili. Kwa mujibu wa Matei (2011), sifa za fasihi simulizi ni kwamba huzaliwa, hukua, huishi na huweza kufa. Anaendelea kusema kuwa kadri jamii inavyobadilika, fasihi simulizi nayo inabadilika na kuathiriwa na maendeleo ya binadamu kisayansi, kijamii na kiteknolojia. Vipera vya fasihi simulizi huzaliwa kutokana na athari za utandawazi, hukuzwa na kupewa uhai katika mazingira mapya.Maoni haya yametupa msukumo wa kufanya utafiti unaohusu fasihi simulizi, hasa fani na maudhui ya nyimbo za harusi mionganini mwa jamii za Wameru na Waswahili, ili kuikuza fasihi hii na kuipa uhai katika mazingira mapya, kwani ulimwengu una mabadiliko mengi mapya yanayosababishwa na uvumbuzi wa kiteknolojia na utandawazi. Uchanganuzi wa nyimbo za harusi za kijadi na zile za kisasa umechangia juhudini zetu za kufufua uhai wa fasihi simulizi.

### **1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti wetu utajikita katika uchambuzi linganishi wa fani na maudhui ya nyimbo za harusi za Wameru na Waswahili. Kama tulivyoangazia katika sehemu ya utangulizi, ni dhahiri kwamba jamii ya Wameru inapatikana katika eneo kubwa la Mashariki mwa Kenya. Hivyo basi,ni vigumu kushughulikia eneo hili pana. Utafiti wetu utajikita katika jamii ya Wameru wa Imenti Kaskazini, inayopakana na Tigania na Imenti ya Kati.Hata hivyo, jamii za Wameru kutoka sehemu mbalimbali wana utamaduni na maadili yaliyo sawa, na vilevile, yanayotofautiana.Haja ikiwemo, tutaweza kutoa mifano kutoka kwa jamii ya Wameru nje ya Imenti Kaskazini.

Kwa vile nyimbo za harusi ni nyingi, tumechagua nyimbo saba katika jamii ya Wameru. Nyimbo hizo zimeteuliwa kulingana na maudhui yaliyomo, fani zilizotumiwa katika kuwasilisha ujumbe na pia umaarufu wake katika sherehe za harusi ya Wameru

Waswahili pia ni wengi na wanaishi katika maeneo mbalimbali. Kulingana na utangulizi wetu, tumeshughulikia jamii ya Waswahili wanaopatikana katika Kisiwa cha Mombasa, wanaotumia lahaja ya Kimvita. Tumechagua Waswahili wa Mombasa kwa kuwa ingawa Waswahili wametanda kwingi katika Pwani ya Kenya, Waswahili wa Mombasa ndio wamo kati ya wale wa kusini na Kaskazini ya Pwani ya Kenya. Tumechagua nyimbo saba tukizingatia maudhui ambayo yamezingatiwa katika nyimbo lengwa, na vilevile fani zilizotumiwa kuwasilisha maudhui hayo. Vile vile tumechagua nyimbo hizo kuambatana na umaarufu wake katika harusi za jamii ya Waswahili. Vipengele vya fani ambavyo tumeshughulikia ni pamoja na toni, matumizi ya lugha, uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, takriri, taswira, kejeli, kinaya na maswali ya balagha.

## **1.6 Msingi wa Kinadharia**

Katika utafiti wetu tumetumia nadharia mbili, kwa kuwa tunalinganisha fani na maudhui ya nyimbo za harusi katika jamii ya Wameru na Waswahili. Mtazamo wa umitindo wa Leech

(1969) umetumiwa katika utafiti wa fani, nayo nadharia ya uhalisia imetumiwa katika uchanganuzi wa maudhui.

### **1.6.1 Mtazamo wa umitindo wa Leech (1969)**

Utafiti wetu umeongozwa na mtazamo wa umitindo wa Leech (1969) katika uchambuzi wa matumizi ya lugha katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili. Leech anaeleza matumizi ya lugha kimtindo katika viwango vitatu vikuu kama ifuatavyo:-

- i. Kiwango cha umbo
- ii. Kiwango cha semantiki
- iii. Kiwango cha utendaji

Kiwango cha umbo kinahusu msamiati uliotumika kujenga sentensi kwa kuegemea mambo ya sarufi na leksika. Ni muhimu mtu kujua msamiati wa lugha na sheria zinazoongoza utungaji wa sentensi. Katika kiwango hiki, tumechunguza uteuzi wa msamiati katika nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili, kama vile uundaji wa maneno mapya, utohozi, mazida, inkisari na kadhalika. Tumechunguza sababu za mwimbaji kuteua msamiati fulani na ufaafu wa msamiati huo katika kazi yake.

Katika kiwango cha semantiki tumeangalia jinsi lugha iliyotumiwa na kuathiri maana kwa njia Fulani katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili, na lugha hiyo inavyoathiri maana ya mwimbaji kwa hadhira. Tumerejelea baadhi ya tamathali za lugha zilizotumiwa na mwimbaji, na ufaafu wa tamathali hizo katika uwasilishaji wa ujumbe au maudhui kwa hadhira lengwa. Kwa mfano, mwimbaji ametumia tashibibi (ulinganishi kwa kutumia maneno kama ‘kama’) ili kusisitiza ujumbe wake, na vile vile kutia mnato au mvuto katika wimbo wake.

Katika kiwango cha utendaji, huwa kunachunguzwa jinsi lugha inavyotamkwa na kuandikwa. Hapa huchunguzwa jinsi lugha inavyotamkwa na waimbaji, hasa wakati wa utafiti wetu wa nyanjani, waimbaji au wahojiwa wanapotuimbia nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili. Baadhi ya wataalamu wamefafanua dhana ya mtindo kama ifuatavyo.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), mtindo ni elementi ya kimsingi katika maana ya jumla ya kazi ya kifasihi. Mwandishi anapoanza kuandika huwa ana maswala anayoyawasilisha kwa wasomaji. Maswala hayo hayawezi kuwafikia wasomaji au kuwa na athari alizonua mwandishi pasipo kuwako na njia ya kuyawasilishia. Njia hiyo kwa jumla ni mtindo. Hii ina maana kuwa hatuwezi kuupuuza mtindo kila tunapoiangalia dhamira. Anaendelea kueleza kuwa mtindo unaakisi njia ya mwandishi au msanii anayehusika na kuyatazama maswala fulani. Ni njia ya kuiwasilisha na kuifumbata tajriba yake, kuupanga na kuuwasilisha welewa au ung’amuvi wake, na kadhalika. Uchunguzi wa mtindo unahusisha mambo mengi kama: uteuzi wa msamiati, miundo ya sentensi, tamathali za usemi, ishara na uashiriaji, jazanda pamoja na hata jinsi anavyoziakikifisha sentensi zake.

Kulingana na Madumulla (2009), kipengele cha lugha huipa fasihi ufasihii wake na kuitofautisha na sanaa nyingine, kama vile uchoraji, uchongaji, ujenzi na ususi. Mtindo unahuusu matumizi ya tamathali za usemi kama vile tashbiha, sitiara, tashihisi, taashira, taniaba, misemo, nahau, methali, uchaguzi wa msamiati, miundo ya sentensi na kadhalika.

Mohamed (1995) anaeleza kuwa mtindo unahuusu namna ya kuitumia lugha ili kuweza kufikia kwa ukamilifu, maana au ujumbe unaotaka kutolewa. Kulingana na Njogu na Chimera (1999) mtindo ni nyezo kuu ya kusanifu kazi nzima. Hii inamaanisha kuwa mtindo ndicho kipengele kinacholeta ujumi katika kazi yoyote ya kifasihi. Hali hii ndiyo inayoiwezesha matini ya kifasihi kuwa ya kusisimua na kumvutia msomaji.

Njogu na Wafula (2002), wanaeleza kwamba madhumuni ya msanii hayawezi kutenganishwa na jinsi msanii huyo anavyowasilisha kazi yake. Kadri mwanafasihii anavyowaza ndivyo vipengele mbalimbali vya kimtindo vinavyomjia. Wanaendelea kueleza kuwa kifasihi, mtindo huelezwa kwa kuanishwa na madhumuni ya msanii. Madhumuni ya dhamira na mtindo ni jinsi dhamira zinavyowasilishwa. Kauli hii inachukuliwa kwamba wazo kwanza huota katika fikra za mwanasanaa, kisha hutumia lugha inayofaa kulieleza wazo hilo.

Mbatiah (2001), anaeleza kuwa fani ni vipengele vya kimtindo na kisanaa vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe na maana mahususi. Naye msokile (1993) anasema kuwa fani ni umbo, ufundi au muundo wa kazi ya kisanna. Senkore (1982), anaeleza fani kuwa ni vipengele vya kisanaa vya kazi ya fasihi vinavyojenga hususani muundo, mandhari, wahusika na lugha. Magara (2015) katika tasnifu yake ya uzamili anafafanua fani kuwa ni jumla ya mbinu, mtindo na nyenzo anazotumia mwandishi katika kuwasilisha maudhui yake na kuipa kazi yake umbo la ndani. Hii ni kauli ambayo imeungwa mkono na wataalamu mbalimbali ambao wameshikilia kuwa fani ni jumla ya viambajengo vya kazi ya fasihi vinavyotumiwa na msanii kupitisha ujumbe wake kwa hadhira. Kitsao (1975), katika tasnifu yake anaeleza kuwa mtindo unaweza kuangaliwa kama jinsi mwandishi au mtunzi anavyojieleza kwa kutumia lugha. Anaeleza kuwa ni kitambulisho cha mwandishi, yaani kila mwandishi hutumia lugha kivyake. Matumizi ya lugha yahusu uteuzi wa vipengele vya lugha kama vile msamiati, sentensi, alama za uakifishi, semi na kadhalika.

Kutokana na fafanuzi zinazotolewa na baadhi ya waandishi wa fasihi, ni dhahiri kuwa ni vipengele vya kimitindo na kisanaa vinavyojenga kiunzi cha kubebbea maana mahususi, yaani ni zile mbinu ambazo msanii anatumia ili kufikisha au kuwasilishaa ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Ni wazi kuwa mtindo unaotumiwa na msanii mmoja ni tofauti kabisa na ule unaotumiwa na msanii mwengine. Hivyo basi maoni yetu ni kuwa kila msanii huwa na mbinu zake za uwasilishaji wa kazi yake ambazo ni tofauti na msanii mwengine, ingawa ujumbe wanaowasilisha huenda ukawa unalingana.

### **1.6.2 Nadharia ya Uhalisia**

Nadharia ya uhalisia inapendekeza kazi ya fasihi iwasilishe maisha ya jamii katika mazingira ya kawaida. Mhalisia anaonyesha ukweli wa mambo katika jamii. Ukweli huo huonekana na kuthibitishwa pasi na taswira yoyote ile; ni uwasilishi wa mambo yanayoonekana wazi katika jamii.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), dhana ya ‘uhalisia’ hutumiwa kwa maana mbili kuu. Kwanza, kueleza tapo la kipindi maalum cha kihistoria katika fasihi za Ulaya. Pili, kueleza aina ya mtazamo au tapo la kifasihi ambako kazi za kifasihi zinachukuliwa kuwa zinazohifadhi au kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisia. Kwa kiasi kikubwa, kazi ambazo zinaangaliwa kama za kihalisia zinatarajiwa kuwa kama akisiko la hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika. Dhana ya uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uamilifu na usahihi mkubwa. Mtazamo huu unatia mkazo kwenye uwasilishi wa mambo yanayoonekana katika jamii.

Msokile (1993) anaeleza tapo la uhalisia kama mtindo wa sanaa wa kuonyesha maisha kama yalivyo na kwamba mambo yaliyotokea katika ulimbwende ndiyo yaliyosababisha kuzuka kwa uhalisia. Anasema kuwa uhalisia ulianza mwaka 1820 B.K. Msingi wa nadharia hii ni kuwa sanaa inatarajiwa iseme ukweli, iwe aminifu na ionyeshe hali halisi ya mazingira. Anapendekeza ujenzi wa wahusika uwe na sura ile ile ya maisha ya kawaida kwani sanaa inafaa ieleze ukweli na iweze kuelewaka. Hivyo basi, dhana ya uhalisia hutumiwa kueleza aina ya mtazamo wa kifasihi unaochukulia kazi za kifasihi kama zinazoakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisia.

Mbatiah (2001) anafafanua uhalisia kama istilahi inayorejelea kimsingi mtindo wa uandishi unaojishughulisha na utoaji wa taswira halisi ya maisha ya kawaida katika jamii mahususi.

Wasanii walioshughulikia tapo hili waliyamini kwamba ukweli uliweza kupatikana katika maisha pamoja na shughuli za kawaida za kila siku za binadamu, akiwa katika mazingira yake halisi ya kijamii. Kutowana na maelezo haya, tunaona kuwa nadharia ya uhalisia hujikita katika ukweli wa hali halisi ya maisha katika jamii mahususi.

Kulingana na Wafula na Njogu, (2007), katika mawanda ya fasihi, uhalisia ultokana na matatizo yaliyokuwa yakiwakibili watu. Matatizo haya yaliwafanya wanasanaa kuutuhumu ulimbwende. Wanaendelea kusema kuwa matamano ya kilimbwende yalikuwa ya kinjozi zaidi yakilinganishwa na taabu zilizokuwa zikiwakibili watu. Walimbwende walijitungia mambo yasiyoweza kutimia. Waliishi ndotoni. Kuanzia mwaka wa 1800 na kuendelea mbele, wahakiki na watunzi walianza kuwadhihaki walimbwende. Gustav Flaubert, mmojawapo wa waanzilishi wa Uhalisia, alishikilia kwamba, “Mtu hufikiria kwa kichwa chake, hafikirii kwa moyo wake”. Flaubert alikuwa akilaani dhana iliyowaongoza walimbwende katika utungaji wao.

Kulingana na maoni ya Rene Wellek katika jarida la Neophilologus, akinukuliwa na Wafula na Njogu (2007), anasema kuwa dhana ya uhalisia ilianza kutumika kwa maana mpya kutokea takriban mnamo mwaka wa 1970. Katika mwaka huo, Emmanuel Kant, katika chapisho lake lilioitwa ‘*critique of judgement*’ alitumia stilahi za udhahania kamilifu kama kinyume cha uhalisia. Kufikia mwaka wa 1978, wahakiki kama vile Schiller walikuwa wakitumia maneno haya, yaani udhanifu (idealism) na uhalisia kuashiria kinyume. Kutowana na historia hii, dhana ya uhalisia imekuja kuhusishwa na miktadha miwili. Kwanza inatumiwa kama njia ya kutathmini hali au halia. Huu ni uhalisia wa maisha. Uhalisia wa kifasihi unaashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali. Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007), kuna baadhi ya mihimili ya uhalisi wa kijamii kama vile:-

- (i) Uhalisi wa kijamii huzingatia masilahi ya makabwela. Hawa ni mafukara wa ulimwengu wenye nia ya kuimarisha udikteta wa makabwela.
- (ii) Binadamu huonyeshwa kiuyakinifu. Wahusika ambao hutumiwa kama vipaza sauti vya watunzi hupuliziwa uhai mathalan wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao.

- (iii) Huonyesha matumaini ya juu ya kizazi cha binadamu. Hii inamanisha kwamba mtu atakuwa mshindi au ni mshindi dhidi ya unyonyaji na unyanyasaji wa aina yoyote.
- (iv) Lughu inayotumika katika uhalisia wa kijamaa inaendeleza malengo na mapendekezo ya walio wengi katika jamii.

Kwa mujibu wa Hegel (1979), katika kitabu chake kinachoitwa *Introduction to Aesthetics*, alitumia neno uhalisia kumaanisha kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikolojia. Msingi mkubwa wa tapo hili ni usimulizi wa ‘kimuhakati’. Huu ni usimulizi ambao unasimulia matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inavyokaribiana sana na hali iliyoko katika jamii. Mwandishi, kwa hivyo, anapaswa kuyaakisi maisha ya kijamii katika ngazi za kijamii, kiuchumi, kitamanduni na kisiasa. Msingi mkuu wa mawazo haya yanaendana na mawazo ya wanafalsafa kama Schelling, ambao wanachukulia kuwa mfanano kati ya jinsi mtu anavyoweza kuyakabili na kuyang’amua mambo , yaani urazini au ung’amuvi wa kibinafsi na uelezeaji wa kihaki. Sanaa inapaswa, kwa kiasi fulani kwenda zaidi ya uwasilishaji wa picha ya uhalisi tu. Wamitia (2003) anakubaliana na Mbatiah (2001) kuwa uhalisia unasawiri matukio ya kila siku katika jamii.

Uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uamilifu na usahihi mkubwa. Mtazamo huu unatia mkazo kwenye uwasilishi wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii. Waandishi wanaoandika kwa msingi huu wanatarajiwa kutoa picha za wahusika, matukio na mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisi wa jamii ya mwandishi anayehusika.

Kwa mujibu wa George Lukacs ( 1978), akinukuliwa na Wafula na Njogu ( 2007), uhalisia ndio lengo kuu la msanii au mwandishi. Mhakiki huyu anaamini kuwa mwandishi anasukumwa na nia ya kuusawiri uhalisi katika ukamilifu wake katika wakati fulani maalum wa kuandika kazi yake. Lukacs anaiona kazi ya msanii au mwandishi kama changamano na yenyewe ukamilifu fulani unaobadilika na wenye sheria au kanuni maalum.

Kulingana na Wafula na Njogu ( 2007), wahusika na wahakiki wengi waliotumia nadharia ya Uhalisia, waliamini ya kwamba dhima ya mwandishi ni kuonyesha ukweli jinsi ulivyo. Kulingana na wataalamu hao, mwandishi anapaswa kuitoa picha ya jamii bila kuidunisha na kuitia chuku. Dhana ya fasihi kuwa ‘ni kioo cha jamii’ilitokana na uhalisia.

Kutokana na maelezo haya, tunaona kuwa nadharia ya uhalisia hujikita katika ukweli wa hali halisi ya maisha katika jamii mahususi. Utafiti wa kiuhalisia hutafiti jinsi mwandishi alivyofanikiwa kudhihirisha ukweli wa mambo kupitia kusawiriwa katika ukamilifu wake. Haya yana umuhimu katika utafiti wetu wa maudhui ya nyimbo za harusi, kwani harusi ni shughuli muhimu katika maisha ya binadamu.

Mbatiah (2001) anasema uhalisia ni tapo la uandishi lililozuka Ulaya katika karne ya kumi na nane na kusambaa katika mataifa mengine ya ulimwengu. Anaendelea kusema kuwa wasanii wa kiuhalisia walijishughulisha kutafuta na kuubainisha ukweli wa maisha ya kila siku ya mwanadamu. Hivyo basi maudhui ya nyimbo za harusi miongoni mwa Wameru na Waswahili husawiri jinsi maisha yalivyo katika mazingira halisi ya jamii.

Ntarangwi (2003) anasema nadharia hii humaanisha uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi na ilizuka katika karne ya kumi na tisa hususan kupinga ulimbwende. Mwanauhalisia huamini kuwa ukweli unaozingatiwa ni ule unaweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajriba. Hivyo uhalisia huwa katika mambo yaliyopo ya matukio halisi kwa matokeo yanayoweza kuthibitika.

Imani ya mhalisia ni kwamba kazi ya fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli na halisi. Mhakiki anayezingatia nadharia hii ya uhalisia hupembua namna mtunzi alivyodhihirisha uhalisi wa mambo kupitia maudhui aliyyozingatia.

Kwa muhtasari, ifuatayo ndiyo mihimili ya nadharia ya uhalisia:-

- i) Kazi za fasihi zinachukuliwa kama zinazohifadhi au kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisia. Kazi hizi zinasawiri hali halisi ya maisha katika jamii husika.

- ii) Wahusika au mhusika hutenda kulingana na jinsi anavyochochewa na hali ya kisaikolojia aliyomo.
- iii) Uhalisia unatoa taswira halisi ya maisha katika jamii mahususi.
- iv) Ukweli unapatikana katika maisha pamoja na shughuli za kawaida za kila siku za binadamu akiwa katika mazingira yake halisi ya kijamii. Mazingira ni lazima yasawiriwe yalivyo bila kutilia chumvi.
- v) Kila kizazi kina uhalisia wake. Uhalisia katika kizazi kimoja unaweza kuwa tofauti katika kizazi kingine.

Kwa kuzingatia maelezo haya tunaona kuwa nadharia ya uhalisia hueleza ukweli wa hali halisi ya maisha ya jamii mahususi. Mtafiti hurejelea jinsi mwandishi alivyofanikiwa kudhihirisha ukweli wa mambo kuitia maswali yaliyopewa kipau mbele. Hivyo basi mtafiti huangalia jinsi ukweli ulivyobainishwa katika lengo la mwandishi ili kufanikisha mawasiliano katika mazingira fulani mahsususi.

Katika utafiti wetu, nadharia ya uhalisia imetatufaa sana katika kuwasilisha ukweli na uhalisi wa ndoa na harusi katika jamii za Wameru na Waswahili, kwani ndoa ni kipera muhimu sana katika maisha ya mwanadamu. Nadharia ya uhalisia inaeleza kuwa mwandishi anapaswa kuitoa picha ya jamii bila kuidunisha wala kutia chuku. Pia mwandishi anafaa kuyaakisi maisha ya jamii katika ngazi ya kijamii, kiuchumi, kitamaduni na kisiasa, jambo ambalo limeangaziwa katika utafiti wetu, kwani harusi ni shughuli ya kitamaduni na vilevile kijamii.

## **1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo la Utafiti**

Nyimbo ni njia asilia na ya jadi ya kutolea mawazo yenyе kina na hisia kubwa, na pia huleta mvuto wa kisanaa na kuufanya ujumbe uwe na msisitizo. Katika utamaduni wa Kiafrika ,nyimbo zilipamba sherehe na tamasha mbalimbali. Nyimbo hizi ni zao la binadamu pamoja na hisia zake na hivyo huzingatia miktadha mbalimbali. Baadhi ya wasomi wameandika mengi kuhusu mada hii.

### **1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nyimbo kwa Jumla**

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996), kuna nyimbo za kazi, za harusi, jando na unyago, ibada na matambiko, maombolezi na nyinginezo. Nyimbo hufungamana na muktadha fulani. Tumetofautiana na kazi yake kwa kuwa utafiti wetu imejikita katika

uchambuzi linganishi wa fani na maudhui ya nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili, bali si aina zote za nyimbo. Kazi hii imetusaidia kupata uelewa wa nyimbo kwa jumla, hasa maudhui ya nyimbo za harusi.

Kirubi (2007), amefanya uchambuzi wa nyimbo kwa jumla, akizingatia muundo wa nyimbo, aina mbalimbali za nyimbo na majukumu ya nyimbo. Kazi hii imetusaidia katika utafiti wetu wa fani na maudhui ya nyimbo za harusi hasa katika uchambuzi linganishi wa maudhui katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili.

Wamitila ( 2003), anasema kuwa nyimbo ni muhimu kwa kuwa zinamwezesha mwimbaji kueleza hisia zinazoambatana na hisia za huzuni , furaha na kadhalika. Nyimbo huburudisha na hutumbuiza watu teule na hufanikisha upataji wa maarifa mbalimbali mionganoni mwa hadhira lengwa. Huwafahamisha watu kutenda mambo fulani au kutenda mengine . Nyimbo huwasilisha hisia nzito na nyeti mtu alizonazo kama vile mapenzi . Kazi hii ni tofauti na yetu kwani tumeshughulikia uchambuzi linganishi wa fani na maudhui katika nyimbo za Kimeru na za Kiswahili. Hata hivyo , kazi hii imetufaa katika uchambuzi wa maudhui ya nyimbo na kuwasilisha hisia nzito kama vile mapenzi kati ya maarusi.

Mbiti (1975), anasema kwamba nyimbo, methali, hekaya na hadithi zinapatikana katika jamii nyingi za Kiafrika. Fani hizi huwa zinatokea katika kipindi maalum na huwa na ujumbe unaobainika katika kipindi hicho. Maoni ya Mbiti yanatunufaisha katika utafiti wetu kwa kuwa yanafafanua kuwa nyimbo hutokea katika kipindi fulani maalum. Mbiti alishughulikia utanzu wa methali, hadithi na hekaya. Utafiti wake unatofautiana na wetu ambao unahusu uchambuzi linganishi wa nyimbo za harusi kwa jamii za Wameru na Waswahili.

Mulokozi (1996), anaelezea kuwa nyimbo hutumiwa kuburudisha watu katika sherehe au wakati wa mapumziko, kuonya, kufunza na kutia hamasa wakati wa vita. Aligawanya nyimbo hizi katika tumbuizo, chapuo, na tendi au tenzi. Alitazama nyimbo zilizoimbwa katika kila mojawapo ya tanzu tatu, na maudhui ya nyimbo hizo kwa hadhira. Maelezo ya Mulokozi yametofautiana na utafiti wetu kwani ametoa maelezo ya nyimbo kwa jumla, ilhali utafiti wetu umejikita katika fani na maudhui ya nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii za Wameru na Waswahili.

Finnegan (1970), kwenye utafiti wa fasihi simulizi katika Afrika amebainisha kuwa nyimbo huimbwa wakati wa kazi mbalimbali na wakati wa sherehe mbalimbali kama vile harusi, uwindaji na kadhalika. Kazi yake imetufaa katika kubainisha nyakati mbalimbali ambazo nyimbo huimbwa. Hata hivyo, kazi yake inatofautiana na utafiti wetu kwani tumejikita katika fani na maudhui ya nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii za Wameru na Waswahili.

Freuchen (1962), akinukuliwa na Finnegan (1970), katika kufafanua maelezo ya nyimbo anasema ni mawazo yanayoimbwa na watu baada ya kusukumwa na nguvu maalum kama vile furaha, hofu, uchaguzi, utulivu na kadhalika. Msukumo huu uliwaapelekea watu kutoa hisia zao kwa kutunga nyimbo mbalimbali.

Senkoro (1987), alichunguza na kuona kuwa chimbuko la nyimbo lilikuwa ni kazi. Wimbo ulimwondolea mtu uchovu na kumpa nguvu ya kufanya kazi. Wimbo ulitumika kuwahamasisha wanajamii kuungana na kufanya kazi kwa ushirikiano. Alitoa maelezo kuhusu umuhimu wa nyimbo katika jamii, tofauti na utafiti wetu unaohusu fani na maudhui ya nyimbo za harusi mionganoni mwa Wameru na Waswahili.

Sunkuli na Miruka (1990), wakinukuliwa na Mulokozi (1996), wameelezea kuhusu nyimbo za nyiso na wanasesma kuwa kusudi la nyimbo hizi ni kuhamasisha waliopashwa tohara kuhusu majukumu yao mapya ya utu uzima, kuwadhihaki waoga, kuwahimiza kuvumilia maumivu ya kimwili, kuuaga utoto na kusisitiza dhima ya utu uzima inayowakabili mabarobaro. Mada yao ni tofauti na yetu kwani wanashughulikia madhumuni ya nyimbo za nyiso kwa ujumla wake, na sisi tumeshughulikia fani na maudhui ya nyimbo za harusi kwa jamii za Wameru na Waswahili.

Beja (2002), amefanya uchambuzi wa nyimbo za matanga katika jamii ya Wagiriamma, ambapo ameshughulikia maudhui. Kazi hii inatusaidia katika kuchambua maudhui ya nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili, hasa za harusi. Hata hivyo kazi ya Beja inatofautiana na utafiti wetu kwani yeye amechambua nyimbo za matanga katika jamii ya Wagiriamma, huku utafiti wetu ukishughulikia uchambuzi linganishi wa fani na maudhui ya nyimbo za harusi katika jamii za Wameru na Waswahili.

Mwai (1997), alitafiti kuhusu nguvu za nyimbo kwa wanawake Waswahili. Alibaini kwamba ingawa wanaume wa jamii ya Waswahili wana uwezo uliokithiri katika ndoa, wanawake wamebuni njia zao za kuelezea hisia zao kama vile maumivu na mateso kupitia kwa nyimbo. Hisia hizi hudhihirika kupitia kwa maudhui katika nyimbo hizi. Kazi hii Imetufaa sana kwani inashughulikia upitishaji wa hisia za mapenzi katika nyimbo za ndoa na vile hisia hizi hujenga maudhui katika nyimbo hizi, nasi tumeshughulikia fani na maudhui ya nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii za Wameru na Waswahili, hasa tulipokuwa tukibainisha maudhui.

Mboti (2012), akimnukuu King'ei (1992) ambaye ameshughulikia lugha, utamaduni na mawasaliano katika nyimbo za taarabu nchini Kenya kati ya mwaka 1963-1990 ni kazi ambayo imetufaa na kutupa mwelekeo kuhusu vipengele vya lugha na tamathali za usemi katika utafiti wetu wa fani na maudhui katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Waweru na Waswahili. Mboti alifanya utafiti uliohusu mtindo katika nyimbo za michezo ya watoto wa darasa la kwanza , katikia tarafa ya Starehe, katika kaunti ya Nairobi.

Kineene wa Mutiso (1985), katika tasnifu yake ya uzamili, ameshughulikia maudhui ya hurafa na uyakinifu katika utenzi wa Hamziyya. Kazi yake imetufaa katika uchambuzi wa fani kwani tumeweza kutathmini jinsi alivyohakiki lugha, hivyo basi ametupa mwelekeo wa jinsi ya kushughulikia kipengele hicho.

Wanjala (1990:91) anasema kuwa, “Nyimbo hutekeleza jukumu maalum katika jamii ya Kiafrika kwa kukuza utangamano mionganoni mwa watu”. Kazi hii ni tofauti na utafiti wetu wa fani na maudhui katika nyimbo za harusi za Wameru na Waswahili, hivyo basi nyimbo zina maudhui mengi bali na kukuza utangamano mionganoni mwa watu.

### **1.7.2. Yaliyoandikwa Kuhusu Nyimbo za Harusi**

Mjomba, (2011), ameshughulikia nadharia ya upole katika kuokoa nyuso za maarusi. Katika uchambuzi wake wa Nyimbo za harusi za Wadawida. Tumeweza kupata ujumbe fiche ambao hautolewi kwa maelezo ya moja kwa moja, hivyo basi, kazi yake imetusaidia katika uchambuzi wa fani katika nyimbo za harusi. Hata hivyo kazi yake ni tofauti na utafiti wetu kwani tumejikita katika uchambuzi linganisha wa fani na maudhui katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili.

Timammy (2002), ameshughulikia nyimbo za harusi za jamii ya Waswahili. Katika kazi yake, Timammy ameshughulikia shughuli za harusi ya Waswahili, posa, uchaguzi wa mchumba,fungate na mengineyo na kasha kuzichambua nyimbo kimitindo. Kazi hii imetusaidia pakubwa katika uchambuzi wa fani na maudhui ya nyimbo za harusi za Waswahili wa Mombasa. Hata hivyo, kazi ya Timammy imetofautiana na utafiti wetu kwani yeze anashughulikia nyimbo za harusi za jamii ya Waswahili, lakini sisi tumejikita katika uchambuzi linganishi wa fani na maudhui katika jamii za Wameru na Waswahili.

Ngome (2014), Ameshughulikia maudhui na majukumu ya bwana na bibi harusi.Kazi hii imetusaidia sana katika uchambuzi wetu wa maudhui ya nyimbo ya harusi katika jamii ya Waswahili, na pia kuangazia tofauti ya kimaudhui na majukumu katika jamii lengwa. Hata hivyo, kazi yake inatofautiana na utafiti wetu kwani tumeshughulikia uchambuzi linganishi wa fani na maudhui katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili.

Kinoti (2008), ameshughulikia nyimbo kwa jumla katika sura ya tano. Amerejelea nyimbo za mapenzi na nyimbo za harusi na kutolea mifano ya nyimbo hizo,hasa katika jamii ya Wameru. Kazi hii imetufaa sana, hasa katika utafiti wetu wa fani na maudhui ya nyimbo za harusi kwa jamii ya Wameru, ambapo tumeangazia utafiti wake wa maudhui ya nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili. Hata , hivyo, kazi yake inatofautiana na utafiti wetu kwani tumeshughulikia uchambuzi linganishi wa fani na maudhui katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili .

Ngure (2003), ameeleza kuwa nyimbo za harusi huimbwa wakati wa furaha katika jamii nyingi, lakini zipo nyimbo pia zinazoimbwa kuelezea masikitiko ya kuondoka kwa binti alikozoea na kwenda asikokujua. Kazi yake imetufaa sana kwani amerejelea kigezo cha kubainisha nyimbo zinazotumiwa katika kumuaga binti, ambacho pia ni kipengele muhimu katika utafiti wetu wa maudhui ya nyimbo za harusi katika jamii ya Wameru na Waswahili.

## **1.8. Mbinu za Utafiti**

Tumetumia mbinu kadhaa za utafiti katika kuutekeleza utafiti wetu

### **1.8.1 Utafiti Maktabani**

Tumetumia vitabu na makala mbalimbali yaliyopatikana katika maktaba. Pia tumetumia baadhi ya tasnifu ambazo ziliandikwa na wasomi mbalimbali wa uzamili na uzamifu katika vyuo, kama vile, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenyatta na Chuo Kikuu cha Kimethodisti, kilichoko mjini Meru. Tumesoma makala ya mtandao yanayotoa maelezo kuhusu fasihi simulizi, hasa utanzu wa nyimbo, ili kupata mwanga zaidi. Tumesoma kazi mbalimbali ambazo zimeandikwa kuhusu nadharia ya uhalisia na pia nadharia ya umitindo kwa lengo la kutupa uelewa zaidi kuhusu nadharia hizi, kwani ni nguzo kuu katika uchambuzi linganishi wa fani na maudhui katika nyimbo za harusi za Wameru na za Waswahili.

### **1.8.2. Utafiti wa Nyanjani.**

Tumehudhuria sherehe za harusi za Wameru na kushuhudia jinsi wanavyotayarisha harusi zao, na utaratibu wa ndoa kwa jumla. Tumepata fursa ya kusikiliza nyimbo za harusi ambazo huimbwa kwa minajili ya kuelekeza, kuonya na kukanya, kupongeza na kuhimiza maarusi kuheshimu ndoa yao. Tumetumia vinasa sauti na simu za rununu katika kurekodi nyimbo hizo, hatimaye tuliandika, kisha kuzifanyia tafsiri katika lugha ya Kiswahili, ili kuweza kuchunguza fani na maudhui yaliyomo.

### **1.8.3. Mahojiano.**

Tumetumia mahojiano ya ana kwa ana na watu wenye tajriba ili tupate maarifa kutoka kwao. Tulikuwa tumeandaa maswali tuliyoyaauliza katika mahojiano. Tuliteua watu wachache ambao walifaa katika kupata maelezo kuhusu jamii ya Wameru na vile vile ya Waswahili. Watu hawa walikuwa makundi mawili, ambao ni vijana walioeleza kuhusu mipango yote ya harusi katika kipindi hiki, na kundi la wazee ambao pia walitueleza utaratibu wa mipango ya harusi ya wakati wao. Uteuzi wa watu hawa umezingatia weledi wao katika maswala ya nyimbo za harusi katika jamii husika. Maelezo na majibu tuliyopata yalihifadhiwa katika kanda za kunasa sauti, na pia simu za rununu. Tuliyaandika maelezo mengine moja kwa moja. Mahojiano ambayo hayakufanywa ana kwa ana yamefanywa kwa njia ya simu au mtandao. Uchanganuzi wa data tuliyokusanya ulifanywa kulingana na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya uhalisia na mtazamo wa umitindo wa Leech ( 1969).

## **SURA YA PILI**

### **MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZA HARUSI ZA KIMERU NA KISWAHILI**

#### **2.0 Utangulizi**

Katika sura hii tumeshughulikia maudhui katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili. Harusi ndiyo sherehe kuu na kilele cha shughuli nzima ya ndoa katika baadhi ya jamii za Kiafrika. Shughuli nyinginezo zinahusu uchumba au posa na mahari. Kwa mujibu wa Nyaga (1986), harusi ya Wameru ilihu VIPENGELE vitatu muhimu, navyo ni uchumba au posa, mahari na harusi. Kulingana na Timammy (2002), harusi ni sherehe muhimu sana hasa kwa Waswahili wa Mombasa. Shughuli ya harusi ilifungamanishwa na sherehe mbalimbali kama vile kupeleka mahari na begi (posa), kueka goma, kutia chooni, kupiga kilemba au kupokea bwana harusi, kung'ara, ushinzi, kupamba, kuosha moo na fungate. Kila sherehe ilikuwa na umuhimu wake kulingana na mila za Waswahili. Hali kadhalika, kila sherehe iliambatana na nyimbo zake maalumu. Hata hivyo, sherehe za kisasa ni tofauti na zile za kitamaduni kutegemea mabadiliko yanayosababishwa na usasa kama vile mabadiliko ya kiuchumi, elimu, ajira na maisha ya mijini.

#### **2.1 Dhana ya Maudhui**

Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999), maudhui ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahuksika au hali ya maisha kama yanavyojitokeza katika kazi ya fasihi, iwe riwaya, tamthilia, shairi au wimbo. Maudhui ni sehemu ya maana na huingiliana na mada. Ni katika maingiliano baina ya mada na maudhui ambapo ukweli uliokusudiwa na mwandishi hujitokeza.

Wamitilia (2002), alieleza kuwa maudhui ni jumla ya maswala na mambo yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi. Katika kuikuza dhamira yake, mwandishi anayaibusha na kuyagusia maswala mengine. Haya ndiyo yanayoitwa maudhui.

Wamitila (2008), anasema kuwa dhana hizi hazipaswi kutenganishwa. Anaendelea kusema kuwa maudhui hayawezi kumfikia msomaji bila ya kuwepo kwa fani, amabayo ni njia kuu ya kuwasilisha maudhui hayo. Katika kitabu chake kingine fani na maudhui ni dhana zinazochangiana na kukamilishana, na hivyo basi, si rahisi

kuzitenganisha katika uhakiki wa kazi ya fasihi. Maudhui hurejelea vipengele mbalimbali kama vile dhamira, ujumbe, mtazamo, msimamo au mwonoulimwengu, falsafa, itikadi na kadhalika.

Kulingana na Mohamed (1995), anaeleza kuwa kazi yoyote ya fasihi ni sharti iwe na sehemu mbili, fani na maudhui. Anasema kuwa maudhui ni jumla ya mambo yanayohusiana na yale mwandishi anakusudia kuyaeleza, na fani ni mbinu ambazo zinatumwiwa katika lugha ili kuyaeleza maudhui na ni stilahi ambazo haziwezi kutenganishwa. Kila siku, fani na maudhui huenda pamoja, kimoja kikisaidia kingine. Fani inayoibuka katika kazi fulani hutegemea maudhui na mwandishi mwenyewe. Katika hali hii, maudhui huongoza fani, yaani fani itakayotumika katika kazi fulani inategemea jinsi ilivyojengwa na mwandishi kwa kuongozwa na matakwa ya maudhui. Upatanisho wa fani na maudhui hivyo basi utapimwa kwa jinsi mwandishi anavyoitumia fani yake kuwasilisha maudhui yake na kulifikia lengo la kuburudisha, kuelimisha au kuonya na kadhalika.

Nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili zilikusudiwa kuwasilisha maudhui kama vile: kutoa mawaidha ya unyumba kwa maarusi wapya; matarajio ya jamii na majukumu ya maarusi; kuonyesha furaha, huzuni au masikitiko kwa upande wa jamii ya bibi harusi baada ya kuachwa na mwanao, anayetwaliwa ugenini; kumhimiza bwana, kuwatayarisha maarusi kwa maisha ya ndoa; kuwasifu maarusi kwa uvumilivu katika ujana wao na kuwashauri dhidi ya changamoto watakazokumbana nazo na jinsi ya kuziepuka na pia kuwasifu wazazi wa maarusi kwa malezi bora kwa wana wao.

Katika utafiti wetu wa uchambuzi linganishi wa maudhui katika nyimbo za Kimeru na Kiswahili, tumezingatia nadharia ya uhalisia, ambayo inapendekeza kazi ya fasihi iwasilishe maisha ya jamii katika mazingira ya kawaida na kwamba mhalisia anaonyesha ukweli wa mambo katika jamii. Ukweli huo huonekana na kuthibitishwa pasi na tashwishi yoyote ile. Ni uwasilishi wa mambo ambayo yanaonekana wazi katika jamii. Kama tulivyogusia katika utangulizi hapo juu, harusi ndiyo sherehe kuu na kilele cha shughuli nzima ya ndoa katika baadhi ya jamii za Kiafrika. Shughuli ya harusi na ndoa kwa jumla huwasilisha ukweli wa jinsi mambo yalivyo katika jamii.

Katika sura ya kwanza ya utafiti wetu, baadhi ya wataalamu wamefafanua nadharia ya uhalisia, akiwemo Mbatiah (2001), anayefafanua uhalisia kama istilahi inayorejelea kimsingi mtindo wa uandishi unaojishughulisha na utoaji wa taswira halisi ya maisha ya kawaida katika jamii mahususi. Harusi ni shughuli ya kawaida na hutekelezwa katika hali halisi ya maisha ya wanajamii.

## **2.2. Maudhui ya Nyimbo za Harusi za Kimeru**

Nyimbo za harusi zinaweza kuimbwa kabla ya harusi, wakati wa harusi au baada ya maarusi kufunga ndoa. Nyimbo hizi hubeba malengo au maudhui mbalimbali. Shughuli mbalimbali za harusi hufungamanishwa na nyimbo tofauti tofauti katika harusi miongoni mwa jamii ya Wameru.

### **2.2.1. Kupongeza / Kusifu Maarusi**

Kuna nyimbo za harusi zinazoimbwa kwa kusudi la kuwapongeza au kuwasifu maarusi, kwa mfano, kwa tabia zao na maadili bora hadi wakati wa kuoana.

Mfano katika wimbo:-

**ii ui kaana ni keega gatuma  
thiora kithioro ii ii nikamenyairwe x 2  
ii ui kaana ni keega gatuma  
thiora kithiora ii ui nikarombairwe x 2**

### **Tafsiri**

Mtoto ni mzuri, aliyeneweza  
kusafiri mabonde na milima paka huku x 2  
Aombewe / atunzwe vyema x 2

Wimbo huu unaimbwaa kwa ajili ya kuonyesha uzuri wa kuwa na mtoto kwani atakapoolewa, atakuwezesha kufunga safari kwenda katika sehemu ambazo hujawahi kufika hapo awali. Wimbo huu pia huwahimiza wazazi kuwatunza na kuwalea wanao vyema, kwani watoto hao watawafaa sana katika siku zao za usoni.

**Mwana ni wa Ncurubi  
ii ii kana ni keega gatuma thiora  
kithioro  
ii ui nikamenyairwe  
Ncurubi iretire mwerine  
Ireja na “mobile” twaragia Amerika.  
ii kana ni keega gatuma  
thiora kithioro  
ii ui nikarombairwe.**

## **Tafsiri**

**Mwana ni wa rika la “Ncurubi”  
ii ui mtoto ni mzuri, atunzwe vyema  
“Ncurubi” ilienda mwezini  
Ikaja na rununu ili tuweza  
kuwasiliana hadi Marekani  
ii ui mtoto ni mzuri, aombewe**

Wimbo huu pia unawapongeza maarusi kwa wao ni wana wa rika la kisasa linalotumia simu za mkono (rununu), kinyume na wana wa rika za hapo awali ambao wamezeeka na mambo yao kupitwa na wakati. Maarusi wanatarajiwa kuwa na maendeleo mengi maishani mwao kiuchumi, kijamii na kimaadili na pia kielimu na siasa.

Wimbo huu pia unawapongeza wazazi wa maarusi kwa kuwalea wana wao vyema:-

### **2.2.2. Ushauri na Mawaidha kwa Maarusi**

Kuna nyimbo za Kimeru zilizoimbwa katika sherehe ya harusi ili kuwashauri na kuwapa maarusi mawaidha katika maisha yao mapya ya ndoa.

#### **Mfano:-**

<b>Kiongozi</b>	<b>:</b>	<b>Garura Mithii.....</b>
<b>Wote</b>	<b>:</b>	<b>Ayia garura mithiire</b>
<b>Kiongozi</b>	<b>:</b>	<b>Ndiunga ya aari</b>
<b>Wote</b>	<b>:</b>	<b>Ayia tigana nayo</b>
<b>Kiongozi</b>	<b>:</b>	<b>Cia eekuru</b>
<b>Wote</b>	<b>:</b>	<b>Ayia ni thaa ikumi</b>
<b>Kiongozi</b>	<b>:</b>	<b>Ng'ombe iri nja</b>
<b>Wote</b>	<b>:</b>	<b>Ayia nigwe mukami</b>
<b>Kiongozi</b>	<b>:</b>	<b>Mukuru uri nja</b>
<b>Wote</b>	<b>:</b>	<b>Ayia nigwe murugiri</b>

#### **Tafsiri**

<b>Kiongozi</b>	<b>:</b>	<b>Badilisha miene.....</b>
<b>Wote</b>	<b>:</b>	<b>Ayia badilisha mienendo</b>
<b>Kiongozi</b>	<b>:</b>	<b>Nyendo za wasichana</b>
<b>Wote</b>	<b>:</b>	<b>Ayia achana nazo</b>
<b>Kiongozi</b>	<b>:</b>	<b>Za akina mama (Kurudi nyumbani)</b>

- Wote** : **Ni saa kumi**  
**Kiongozi** : **Ng'ombe aliye humu**  
**Wote** : **Ayia ndiwe wa kukamua**  
**Kiongozi** : **Bwana aliye humu**  
**Wote** : **Ayia ndiye wa kumpikia**

Katika wimbo huu, mashauri na mawaidha yanaelekezwa kwa bibi harusi. Anashauriwa kwamba mienendo aliyokuwa nayo kabla ya kuolewa na ushirikiano wake na wasichana ufkishwe mwisho, abadilishe na kuiga mienendo ya akina mama. Anaonywa kuwa saa ya akina mama kurejea nymbani ni saa kumi ili waweze kutekeleza majukumu ya nyumbani kama vile kukamua ng'ombe na kuwapikia mume na watoto. Ushauri na mawaidha mengine pia yaliwasilishwa kwa maarusi.

Katika wimbo **Gikubwa kiatho**, bibi harusi anashauriwa kuwa na heshima kwa wazazi wa mumewe . Anapomwona mama mkwe, alitarajiwa kumwita ‘mama’ na vile vile baba mkwe anapaswa kumwita ‘baba’.

Bwana harusi naye anashauriwa kuwaheshimu wazazi wa mke wake na kuwatembelea mara kwa mara, kwani wao pia ni wazazi wake.

- Kiongozi** : **Wona ng'ina wa nthaka mwitage mami**  
**Wote** : **Gikubwa ii gikubwa kiatho**
- Kiongozi** : **Onagwe mugurani utigatire kwaba**  
**Wote** : **Mwari Gikubwa ii Gikubwa kiatho**

### **Tafsiri**

- Kiongozi** : **Bibi harusi ukimwona mama mkwe umwite  
mama imefana ee**  
**Wote** : **Imefana harusi**  
**Kiongozi** : **Na wewe bwana harusi usisite  
Kutembelea wazazi wakwe**  
**Wote** : **Imefana harusi.**

Wimbo huu unaendelea kumshauri bibi harusi kuwa ndiye atakayefua nguo za mumewe. Bwana harusi naye anafahamishwa kuwa amempata mpishi na mchungaji wa ng'ombe wake, hivyo basi anatarajiwa kumpenda na kumtunza vizuri. Mama mkwe naye anafahamishwa kuwa atapikiwa chai ya “Ovatini” na “milo” na bibi harusi. Ushauri huu unaegemea katika nadharia ya uhalisia ambayo inahimiza usawiri wa hali ya maisha ya kawaida. Katika jamii ya Waweru , bibi anatarajiwa kuwajibika na kutekeleza baadhi ya majukumu . Haya ni mambo ya kawaida katika jamii.

- |                 |   |  |
|-----------------|---|--|
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Na nguo cia muthaka nigwe</b>         |
|                 |   | <b>Ukauragi giikubwa ii</b>              |
| <b>Wote</b>     | : | <b>Giikubwa kiatho</b>                   |
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Ukwona murugi, mutwiri wa ng'ombe</b> |
|                 |   | <b>Giikubwa ii</b>                       |
| <b>Wote</b>     | : | <b>Giikubwa kiatho</b>                   |
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Na kinya gwe ngino nthaka</b>         |
|                 |   | <b>Ukanyua obatini ya milo</b>           |
| <b>Wote</b>     | : | <b>Giikubwa kiatho</b>                   |
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Urugiri ni muko mutana giikubwa</b>   |
| <b>Wote</b>     | : | <b>Giikubwa kiatho</b>                   |

### Tafsiri

- |                 |   |                                    |
|-----------------|---|------------------------------------|
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Ndiwe utafua nguo za mumeo</b>  |
| <b>Wote</b>     | : | <b>Imefana ee</b>                  |
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Umepata mpishi na mchungaji</b> |
|                 |   | <b>ng'ombe wamefana ee</b>         |
| <b>Wote</b>     | : | <b>wamefana ee</b>                 |
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Mama mkwe atapikiwa</b>         |
|                 |   | <b>Chai ya “Ovatin na milo”</b>    |
| <b>Wote</b>     | : | <b>Imefana ee</b>                  |

Nyimbo hizi za kuelekeza au kutoa ushauri ziliimbwa na akina mama ambao waliniua kumweleza bibi harusi baadhi ya majukumu atakayotarajiwa kuzingatia katika ndoa

yake. Ushauri wa bwana harusi pia ultajwa. Hivyo basi, ushauri na mawaidha kwa maarusi yalitolewa katika kila nyanja ya maisha yao. Ushauri huu uliwawezesha maarusi kufikia ufanisi wa hali ya juu katika maisha yao ya ndoa.

Ushauri na mawaidha kwa maarusi lilikuwa ni jambo lililotiliwa maanani sana katika jamii ya Wameru. Siku ya harusi ilipowadia, mamake bibi harusi aliwaandalia sherehe kina mama wa rika lake nyumbani kwake ili wampe mawaidha binti yake. Baadhi ya mawaidha yaliyopendekezwa ni kama vile:-

- ❖ Kuwatii na kuwaheshimu wazazi wakwe
- ❖ Kumtii mumewe na kumheshimu sana
- ❖ Kuweka siri mambo ya kinyumbani
- ❖ Kutulia nyumbani kwake na kutekeleza majukumu ya mke nyumbani ipasavyo
- ❖ Kutomchapa mtoto machoni mwa somoye.

Mamake bibi harusi pia alimpa mawaidha bintiye. Alimhimiza kila asubuhi ambariki mumewe alipotoka kwenda katika shughuli zake, na daima dawamu asidhubutu kumtusi au kunung'unika juu ya mumewe. Alimkumbusha jukumu lake la kuwatunza na kuwaheshimu wazazi wa mumewe, kwa mfano kuwapelekea vyakula. Vile vile, alimwambia bintiye kuhusu kuwaheshimu watu wote wa jamii ya mumewe. Bibi harusi pia alikanywa dhidi ya kushiriki ngono nje ya ndoa. Msichana alitarajiwa kutunza ubikira wake hadi siku ya harusi. Msichana ambaye alivunja ubikira wake alichukuliwa kuwa mke mkware, na hakuolewa kwa sherehe za harusi. Pia aliweza tu kuolewa kama mke wa pili au wa tatu na mtu au mume asiyeheshimika katika jamii.

### **2.2.3. Kufana kwa Harusi**

Kwa mujibu wa Kinoti (2008), kilele cha harusi ya Wameru ni wimbo mashuhuri wa kushangilia na kushereheke harusi ya kufana sana. Wimbo huu huimbwa na akina mama na pia akina baba baada ya kuridhishwa na sherehe. Iwapo wimbo huu hauimbwi, hii ni ishara kwamba mambo ni mabaya.

### **Mfano:**

- |                 |   |   |
|-----------------|---|---|
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Giikubua ii ii</b>                                     |
| <b>Wote</b>     | : | <b>Gikubua ii Gikubua kiatho</b>                          |
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Kiatho kia mwanetu gikubua ii</b>                      |
| <b>Wote</b>     | : | <b>Gikubua ii Gikubua ii Gikubua kiatho</b>               |
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Muiki twinawe giikubua ii ii</b>                       |
| <b>Wote</b>     | : | <b>Giikubua ii ii Gikubua ii</b><br><b>Gikubua kiatho</b> |

### **Tafsiri**

- |                 |   |                                      |
|-----------------|---|--------------------------------------|
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Imefana ee</b>                    |
| <b>Wote</b>     | : | <b>Imefana harusi</b>                |
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Imefana ee</b>                    |
| <b>Wote</b>     | : | <b>Imefana sherehe</b>               |
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Sherehe ya mwanetu imefana ee</b> |
| <b>Wote</b>     | : | <b>Imefana ee</b>                    |
| <b>Kiongozi</b> | : | <b>Tunaye bibi harusi ee</b>         |
| <b>Wote</b>     | : | <b>Imefana ee</b>                    |

Wimbo huu ulikusudiwa kudhihirisha ufanisi wa sherehe ya harusi na kwamba akina mama walifurahia kuwa na bibi harusi mionganini mwao. Wimbo huu uliimbwa na watu wote waliohudhuria sherehe ya harusi, wake kwa waume, wote wakiwa wameketi.

#### **2.2.4. Kuomba Msamaha**

Siku ya harusi inapowadia, wazazi na jamii ya upande wa mvulana huandamana hadi nyumbani kwa msichana au bibi harusi ili kuomba kupewa bibi harusi ili wampeleke kanisani kwa ibada takatifu la ndoa. Iwapo wazazi wa bwana harusi walichelewa kufika kwa boma la wazazi wa bibi harusi, wanatarajiwa kuomba msamaha kwa unyenyeketu ili wasiwaudhi wazazi wa bibi harusi. Wimbo wa kuomba msamaha uliimbwa na jamii ya bwana harusi pindi tu walipowasili nyumbani kwa bibi harusi:-

**Mbirira muthoni ntigucereri**  
**Ni mbotiki ngwikaira ibungo**

**Mpumite kuraja tigucereri**  
**Mucii jwa muthoni ntigucereri**

**Tafsiri**

**Waambie shemeji wetu kuwa**  
**hatujachelewa kwa ubaya**  
**Ni nguo za “Boutique” (Jumba la kuuzia nguo)**  
**tulikuwa tukishonelea vifungo.**

**Waambie shemeji wetu kuwa**  
**Hatujachelewa kwa ubaya**  
**bali tumetoka mbali sana.**

Wimbo huu uliimbwa na wazazi wa bwana harusi ili kuomba msamaha kwa kufika nyumbani kwa akina bibi harusi wakiwa wamechelewa. Wimbo unaelezea kuwa kuchelewa kwao kulisababishwa na shughuli ya kushonelea vifungo kwenye nguo zao mpya za harusi ('za Boutique'). Wanaendelea kukiri na kuungama kuwa kutoka kwao hadi kwa wazazi wa bibi harusi ni mbali, hivyo basi hawakuwa na budi kuchelewa.

Wimbo huu unanuia kuonyesha kwamba wazazi wa bwana harusi walipaswa kuwaheshimu wazazi wa bibi harusi, hasa kwa kuwapa bibi harusi, hivyo basi hawakutarajiwa kukosa heshima kwa vyovyyote vile. Pindi walipowasili, walitarajiwa kuomba msamaha kwa unyenyekevu. Wakati mwingine, na kulingana na hasira ya wazazi na jamii ya bibi harusi, wazazi wa bwana harusi walilazimika kutoa faini au pesa kiasi fulani kama kitulizo kwa wazazi wa bibi harusi. Hata hivyo, kusutana kwa familia zote mbili lilikuwa ni jambo la kimzaha tu bali si kukasirikiana.

### **2.2.5. Kutahadharisha**

Nyimbo za harusi huimbwa kwa kusudi la kutahadharisha au kukanya dhidi ya kutekeleza vitendo visivyofaa. Wimbo unawenza kuwatahadharisha maarusi, wazazi wa pande zote mbili, wasimamizi wa harusi au marafiki wa maarusi dhidi ya matendo yasiyofaa. Wimbo ufuatao ni mfano wa tahadhari kwa wazazi wa bwana harusi.

**Kiongozi : Mwana ti mbetiri atuura ngarine**

**Wote : Mwana ti mbetiri atuura ngarine**

**Kiongozi : Mwana ti ncaabi arara gwakirua**

**Wote : Mwana ti ncaabi arara gwakirua.**

**Kiongozi : Mwana ti mwere atindua maegone**

**Wote : Mwana ti mwere atindua maegone.**

### **Tafsiri**

**Kiongozi : Mtoto sio betri aishi kwa gari**

**Mtoto sio maharagwe apikwe usiku kucha.**

**Mtoto si maweles ashinde kwenye kinyua kutafunwa**

Wimbo huu unaimbwaa baada ya maarusi kuwasili nyumbani kwa bwana harusi katika hatua ya kuwatoa maarusi kwenye gari. Wimbo huu hukusudiwa kumharakisha babake au kaka zake bwana harusi ili watoe zawadi ya kumkaribisha bibi harusi. Zawadi hii huwa ni ng'ombe jike. Babake bwana harusi anatahadharishwa kuwa amtoe bibi harusi haraka kutoka kwa gari, kwani mtoto sio betri ya gari iishiyio kwenye gari, mtoto si maharagwe yanayotiwa motoni usiku kucha wala mtoto si maweles ashinde kwenye meno akitafunwa

### **2.2.6. Kumkaribisha Bibi Harusi Nyumbani**

Kuna nyimbo za harusi ambazo husheheni maudhui ya kumkaribisha bibi harusi nyumbani kwa bwana harusi.

Mfano katika wimbo:-

**Mbirira Karuthu arete rubunguro**

**Nyomba ya mutana ikwona muruguri x 2**

## **Tafsiri**

**Mwambie mamamkwe alête ufunguo  
Nyumba ya bwana harusi imepata  
wa kufungua.**

Wimbo huu unaimbwaa jioni baada ya kumalizika kwa sherehe ya harusi kwa kusudi la kumpeleka bibi harusi katika nyumba ya bwana harusi. Wanawake huongoza bwana na bibi harusi kuelekea kwenye nyumba yao. Mama mkwe anafahamishwa kwamba nyumba ya bwana harusi imepata mtu wa kuifungua, hivyo basi, ilimbidi atoe ufunguo, kwa bibi harusi ambaye kuanzia siku hiyo ya harusi, ndiye mwenye nyumba. Wimbo huu pia unanua kumtahadharisha mama mkwe dhidi ya kuingia kwenye nyumba ya bwana harusi. Maana maalumu ya tahadhari hii ni kuwa ni jambo la aibu kwa mama mkwe kuingia katika nyumba ya bwana harusi kwani maarusi walitarajiwa kushiriki ngono, na ingekuwa aibu kubwa kwa mama mkwe kushuhudia tendo hilo. Hakuna watu wengine wanaoruhusiwa kuingia katika nyumba hii, ila maarusi na wasimamizi wao wa harusi. Wasimamizi hawa walitarajiwa kutoa mwongozo wa maisha ya ndoa kwa maarusi. Mama mkwe anatarajiwa kumkabidhi bibi harusi zawadi kama ukaribisho rasmi katika nyumba yake.

### **2.2.7. Maudhui ya Kukejeli**

Kukejeli ni kumwambia mtu maneno yenyeye dharau, kufanya mzaha au kukebehi. Katika harusi ya Kimeru, nyimbo zenye kejeli ziliimbwa, hasa na wanawake wa upande wa bwana harusi walioimba nyimbo za kukejeli wanawake wa upande wa bibi harusi, wakiwaambia kwamba wamemla mwana wao wa kike vizuri na kwa kuwa wamemchukua, walitakiwa kumlea mwingine au wengine ili waje wawachukue pia. Wakati wa kumkaribisha bibi harusi nyumbani, wanawake pia huimba wimbo kumkejeli babake bwana harusi kuwa asikawie kumzawadi bibi harusi na kumtoa kwenye gari kwani mtoto si betri ya gari iishiyo kwenye gari, au maharagwe yatiwayo mekonii usiku kucha, ama mawele ambayo hushinda kinywani yakitafunwa kwa sababu ya ugumu wake.

**Mwana timbetri atuura ngarine  
Mwana ti mbetri atuura ngarine**

**Mwana ti ncaabi araara gwakirua**  
**Mwana ti ncaabi araara gwakirua.**

### **Tafsiri**

**Mtoto si betri inayoishi kwa gari**  
**Mtoto si maharagwe apikwe usiku kucha.**

### **2.2.8. Maudhui ya Kuburudisha**

Kuburudisha ni hali ya kufurahisha, kuchangamsha na kuondolea watu uchovu. Burudani katika nyimbo hutuliza akili za hadhira. Nyimbo nyingi za Kimeru zinasheheni haya. Nyimbo za burudani huimbwa hasa watu wanapopokea vyakula, wakati wa kukata keki au wakati wa kutoa zawadi kwa maarusi. Nyimbo hizi pia huimbwa kanisani wakati wa kuwasubiri maarusi kula yamini au kiapo cha ndoa au baada ya ibada ya ndoa. Ufuatao ni mfano wa wimbo unaotumbuiza watu wakati wa kupokea chakula, au jioni baada ya sherehe ya harusi.

**Iririri nandi ii iriri nandi x 2**  
**Kinanda igikuchue ii iririri nandi**  
**Kienda gutwika nigituike**  
    **ii iririri nandi**  
**Muthaka agure kingi**  
    **ii iririri nandi**  
**Twinire muiki**  
    **ii iririri nandi**  
**Muuiki wina neti**  
    **ii iririri nandi**

### **Tafsiri**

**Iririri leo ii iririri leo**  
**Kinanda kichezwe**  
**Waya ukikatika wacha ukatike**  
**Bwana harusi anunue kingine**  
**Tumchezee bibi arusi**  
**Bibi harusi aliye na neti**  
**Bibi harusi aliye na neti**  
**Iririri leo ii iririri leo**

Wimbo huu unasema kwamba leo ni leo, ambayo ni siku kuu ya sherehe ya harusi. Watu wote wanaambiwa wajikakamue washike kinanda au chombo cha mziki ili wacheze, hata kama nyaya zitakatika, bwana harusi atanunua kinanda kingine. Wimbo huu unasisitiza hali ya furaha ambayo hadhira, pamoja na waimbaji kwa kumpata bibi harusi. Nyimbo za burudani huimbwa na hadhira yote, wakati mwingine maarusi na wasimamizi wao wakiongoza huku watu wengine wakiwafuata na kuunda duara kubwa uwanjani. Watu huzunguka katika hali ya mviringo huku wacheza vyombo vya mziki wakivicheza vyombo mbali mbali. Fani za kiutendi kama vile minenguo ya mwili hushirikishwa. Katika mpangilio huo wa duara na maarusi wakiongoza, inaaminika kwamba ni gari la moshi, ambalo limebeba hadhira nzima chini ya uongozi wa madereva wawili, bwana na bibi harusi. Hiki ndicho huwa ni kilele cha tumbuizo au burudani katika harusi ya Kimeru.

#### **2.7.9. Maudhui ya Maombi / Dua**

Kwa kurejelea utafiti wetu, tumeona kuwa baadhi ya nyimbo za harusi za Kimeru husheheni maudhui ya maombi au dua.

Katika wimbo wa **Mwana ti mbetiri** ujumbe unawasilishwa kwa maarusi kuwa hakuna chochote cha kuwaogofya maishani, kwani Mungu yu pamoja nao na anawaongoza, na kwamba Mungu yuyu huyu ndiye wameishi kumwomba kwamba awatunukie baraka zake.

Mfano katika wimbo:-

**Murungu arokumwa ui**  
**Acore betu ui ii**  
**Tutwire kuromba**  
**Mwana ti mbetiri atinda ngarine**

#### **Tafsiri**

**Mungu apewe sifa**  
**Marafiki zetu wote**  
**Tumeshinda tukiomba wakati wote.**  
**Mtoto ti mbetri ashinde kwa gari**

Ni vyema kusisitiza kuwa maudhui ya maombi yalipewa kipao mbele hata katika siku za jadi. Baada ya kujenga nyumba ya bibi harusi asubuhi ya siku ya harusi, maombi ya kutakasa maarusi na nyumba yao yalifanywa kabla ya maarusi kuingia katika nyumba hiyo. Waliombewa kuwa na jamii bora iliyobarikiwa na watoto, kilimo, ufgugaji na kadhalika. Maarusi walitunukiwa zawadi hasa na wazazi wao.

#### **2.7.10. Maudhui ya Majukumu ya Maarusi**

Baadhi ya nyimbo za harusi za Kimeru zilikusudia kuwaelekeza maarusi katika majukumu yao katika maisha yao ya ndoa.

Katika wimbo wa **Garura Mithiire** bibi harusi anaelekezwa kwamba ana jukumu la kurejea nyumbani mapema (saa kumi) kama ilivyo desturi ya mama, ili aweze kukamua ng'ombe na kumpikia mumewe na watoto. Pia alitarajiwu kuwatunza wazazi wa mumewe au wakwe, kwa mfano, kuwatengenezea uji na vyakula vinginevyo. Vile vile, bibi harusi alikuwa na jukumu la kulima na kupanda kwenye shamba lake.

<b>Kiongozi</b>	:	<b>Ng'ombe iri njaa</b>
<b>Wote</b>	:	<b>Ayia nigwe mukami</b>
<b>Kiongozi</b>	:	<b>Mukuru uri nja</b>
<b>Wote</b>	:	<b>Ayia nigwe murugiri</b>
<b>Kiongozi</b>	:	<b>Ngino nthaka</b>
<b>Wote</b>	:	<b>Ayia nigwe mumenyeri</b>
<b>Kiongozi</b>	:	<b>Ucuru bwao</b>
<b>Wote</b>	:	<b>Ayia nigwe mukii</b>

#### **Tafsiri**

Bibi harusi ndiye atakamua ng'ombe  
Bibi harusi ndiye atapikia jamii yake  
Bibi harusi ndiye atawatunza wazazi wakwe.

Wimbo wa **Gikubwa Kiatho** pia unaeleza baadhi ya majukumu ya maarusi. Bibi harusi anashauriwa kuwa ni jukumu lake kuwashemeshimtu wazazi wakwe na kuwatunza kwa kuwapatia chakula. Pia alitarajiwu kumheshimtu mumewe na kumtimizia

mahitaji yake yote. Bibi harusi alikuwa na jukumu la kumfulia mumewe nguo, kuwalisha na kukamua ng'ombe na kushughulikia shamba lake.

**Wona ngino nthaka umwitage ‘maami’**

**Gikubwa ii Gikubwa kiatho**

**Na nguo cia muthaka nigwe ukauraga**

**Gikubwa ii Gikubwa kiatho**

**Ukwona murugi na mutwiri wa ng'ombe**

**Gikubwa ii gikubwa kiatho.**

### **Tafsiri**

**Umwonapo Mamamkwe umwite ‘mama’**

**Harusi imefana sana**

**Nguo za mumeo ni wewe utafua**

**Harusi imefana sana umepata mpishi na mfugaji wa ng'ombe**

**Harusi imefana sana.**

Bwana harusi pia anashauriwa kuwa ni jukumu lake kuwatemelea wazazi wakwe, kuwaheshimu na kuwatuza kwani ndio waliompatia ubavu wake. Ni jukumu la bwana harusi kumpenda mkewe na kukimu familia yake vyema.

**Utigatiire kwa ba mwari.**

**Gikubwa ii Gikubwa kiatho.**

**Nibo bakua rwaru rwaku rwa urio**

**Gikubwa ii Gikubwa kiatho.**

### **Tafsiri**

**Usikose kuwatemelea wakwe wako**

**Harusi imefana sana**

**Ndio waliokupa ubavu wako wa kushoto**

**Harusi imefana sana**

### **2.3. Maudhui ya Nyimbo za Harusi za Kiswahili**

Harusi ndicho kilele cha shughuli zote za ndoa katika jamii ya Waswahili, kama ilivyokuwa katika baadhi ya jamii za Kiafrika. Harusi huwa na sherehe mbalimbali, na kila sherehe hufangamanishwa na nyimbo zake maalum. Nyimbo hizi huwasilisha maudhui kwa maarusi au wazazi. Maudhui haya ni kama vile ushauri kwa maarusi, mapenzi, maombi, vijembe, pongezi au kukashifu, majukumu ya maarusi na mengineyo. Katika sehemu hii, tumeshughulikia baadhi ya maudhui yanayowasilishwa katika nyimbo za harusi za Wakiswahili.

#### **2.3.1 Maudhui ya Maombi / Dua**

Wakati wa harusi ya Waswahili, kuna nyimbo ambazo zinainmbwa kwa kusudi la kuwaombea maarusi mema na baraka za Mungu. Kwa mfano, katika nyimbo za **Qasida za Harusi**, waimbaji ni wanaume wa makamo wa rika la bwana harusi, ambao huvalia mavazi ya Kiislamu na kuketi pamoja na bwana harusi huku wakimwimbia. Huu ni wimbo wa kiutendi, ambapo baadhi ya matendo hufanywa, kama vile kusonga kwa upande mmoja na kisha upande mwingine, kuinamisha nyuso zao , kupiga makofi na kadhalika

Wimbo huu unawaombea maarusi dua njema kwa Mwenyezi Mungu. Kwa mfano:-

**Bwana harusi na bibi arusi**

**Nuru na kheri iwashukie x 2**

**Kwa radhi za Mtume**

**Waishi daima kufanya mema x 2**

**na watoto wao Mola awajalie**

**Nuru ya kheri iwashukie**

**Fahamu nzuri uwabarikie**

Maarusi wanaombewa maisha mema katika ndoa yao ya kheri, na kwamba Mungu awabariki na watoto wenye fahamu nzuri. Katika wimbo wa harusi wa **Salaam Bwana Kharousi** maarusi wanaombewa Mungu awabariki na awasaidie waishi maisha mema.

**Kwa bwana Kharousi aishi Salama**

**Na bibi harusi twawaombea mema.**

**Wameshatimiza jambo lenye maana  
Alilohusia mtume heshima.**

Kulingana na watu waliohojiwa, mambo ya kidini yalipewa kipao mbele hasa katika harusi za hapo jadi. Kulingana na mila na desturi za Waswahili, wazazi ndio walitoa uamuzi wa mchumba wa msichana au mvulana, na hata mahari yatakoyotolewa na wala, hakuna aliyeweza kupinga uamuzi wao. Msichana pia aliweza kuamua mahari yake kuwa kitakatifu cha Korani na mswala.

Mahari na zawadi zilizotolewa zilikuwa kulingana na dini ya Kiislamu iliyotilia mkazo kupeana zawadi kama njia ya kuhimiza mapenzi kati ya wanajamii. Kauli hizi zinadhahirisha kuwa mambo ya kidini na maombi lilikuwa ni jambo lililozingatiwa sana katika harusi za Waswahili.

**2.3.2. Ushauri kwa Maarusi**

Nyimbo pia hukusudia kutoa ushauri kwa maarusi wakati wa ndoa yao. Katika wimbo wa Usiche maarusi, maarusi wanapewa ushauri. Bwana harusi anaambiwa asiogope chochote maishani. Anaendelea kushauriwa kuwa akiona bahari ataiogelea hadi avuke bahari. Bibi harusi naye anashauriwa kuwa asiogope chochote, na bwana harusi akitaka tafadhali ampe. Huu ni ushauri uliofumbatwa katika fumbo, ukinuia kuwashauri maarusi kuhusu kushiriki ngono au mambo ya kimapenzi. Wote wawili wanashauriwa wasiogope na kwamba wawili washiriki ngono bila kuogopana au mmoja kukosa kutimiza matakwa ya mwengine.

**Usiche bwana harusi usiche  
Usiche bwana harusi usiche  
Ukiona bahari utaogelea  
Usiche bahari utaogelea uvuke  
Usiche bibi harusi usiche  
Usiche bibi harusi usiche  
Bwana akitaka tafadhali mpe.**

Katika wimbo wa **Qasida ya harusi ya Hamisa Obeid**, maarusi wanashauriwa waishi kufanya mema kwa radhi za Mtume.

**Kwa radhi za mtume**  
**Waishi kufanya mema**

Katika wimbo wa **Kheri ishallah** maarusi wanashauriwa wakae au waishi milele wakizingatia sheria za Kiislamu. Wanaendelea kushauriwa kuwa kwa baraka za Mtume, wazae mke na mume na kwa baraka za Mungu maisha yao yawe mazuri.

**Wakae hadi milele**  
**Kwa sheria za Kiislamu**  
**Kwa Baraka za Mtume**  
**wazae mke na mume**  
**Kwa Baraka za rasuly**  
**Maisha yawe mazuri**

Wimbo huu unaendelea kuwaombea kwa Mungu awahifadhi na maovu yaliopo na kwa kuwa wamependana, waendelee kupalilia mapenzi yao, kwani upendo ndio uliwaapelekea kuoana.

**Wahifadhi ya Qahari mabaya yalokithiri**  
**Kwa kweli wamependana**  
**Ndio maana wakaoana.**

Ni dhahiri kuwa ushauri kwa maarusi lilikuwa jambo lililotiliwa maanani sana katika ndoa ya Waswahili. Katika sherehe iliyojulikana kama kufuga ukuti, mwanamwali alitiwa ndani kwa kupindi cha majuma au muda ambao hakuruhusiwa kutoka nje kwa kipindi chote cha matayarisho ya harusi. Alipewa mafunzo na kungwi aliyejikuwa mtaalamu wa masuala ya unyumba kati ya mume na mke. Huyo kungwi alikuwa mama mzee. Alifundisha kuhusu usafi wa mwili, unadhifu na jinsi ya kumstarehesha mume kimapenzi. Vile vile, kulikuwa na somo ambaye alikuwa mtaalamu wa maswala ya elimu asilia ya Waswahili na ndoa. Katika kuwahoji watu tuliochagua ili wahojiwe kuhusu harusi ya Waswahili walitueleza kuwa katika kipindi cha kufuga ukuti, somo alitarajiwa kumpaka bibi harusi mafuta kwenye ngozi na nywele na kumtoa nywele za malaika katika mwili wake na kumfuta uso ili bibi harusi aonekane

mrembo. Haya yanadhihirisha kuwa maudhui ya ushauri kwa maarusi lilikuwa jambo ambalo lilisisitizwa sana.

Katika wimbo wa **Harusi wa Issa Matona**, msanii anawaita makungwi pamoja na mama harusi ili wamsaidie katika kumpa ushauri bibi harusi. Msanii anawaambie waje wamfunze mwali aache kufedheheka. Bibi harusi anashauriwa kuwa aitwapo na mumewe aitikie ‘ labeka’ ili kuonyesha heshima. Bibi harusi anashauriwa kuwa ni wajibu wake kumrithia mume wake kwa kila jambo alilolitaka. Wakati mume wake atakapowasili nyumbani bibi harusi anashauriwa. Kuwa ni heri wasalimiane kwa furaha kisha amchukulie mume wake mkoba.

**Yu wapi mama harusi aje tumfunze mwali  
Aache kufedheheka.  
Akiitwa na mumewe wajibu kuitikia ‘ labeka’  
Umrithie mumeo kwa kila analotaka.**

### **2.3.3 Maudhui ya Kuwashimiza Maarusi**

Nyimbo za harusi za Waiswahili hunuia kuwashimiza na kuwatia shime maarusi hasa wanapoanza maisha yao mapya katika ndoa. Katika wimbo wa **Qasida ya Harusi wa Hamisi Obeid**, msanii anawahimiza maarusi kwamba harusi ni njema na ni kitendo kinachofurahiwa na watu wote katika jamii, hivyo basi, anawahimiza kufanikisha ndoa yao.

**Harusi ni sunnaaa njema  
Minn sunnaa  
Kitendo cha watu fiii ummaa  
Ndoa kwetu ni halali minn Sunnaa  
Ni jambo jamili ii fiii ummaa**

Kwa kurejelea wimbo wa **Harusi wa Issa Matona**, msanii anamhimisa bibi harusi kwa kumpa hongera kwa ufanisi wa harusi, kisha msanii anawaita watu mbalimbali ili waingie uwanjani na kucheza wimbo pamoja na bibi harusi. Anawaita watu kama vile mamaye bibi harusi, dadake bibi harusi, somo yake

bibi harusi na shangazi yake bibi harusi . Anawaambia waje ili wahangaike na  
bibi harusi maana yake ni kuwa waende wacheza na kumhimiza bibi harusi

Mfano katika wimbo:-

**Hongera mwanangu**

**Hongera mwanangu**

**Sisi wazazi asema yu wapi mama harusu**

**Aje hapa tuhangaike naye x 4**

**Shangazi yake harua naye nataka aje hapa**

**Tuhangaike naye**

**Na dadake harusi naye nataka aje hapa**

**Na Somo yake harusi nataka aje hapa**

**Tuhangaike naye**

**Bibi yake harusi nataka aje hapa**

**Tuhangaike naye**

**(Aje hapa tuhangaike naye x4)**

#### **2.3.4 Majukumu ya Maarusi**

Nyimbo za harusi za Waswahili zinanuia kuwahamasisha maarusi dhidi ya majukumu  
yao katika maisha ya ndoa. Majukumu haya ni kama yafuatayo:-

##### **2.3.4.1 Makazi Mema**

Bwana harusi alitarajiwa kumpa bibi harusi makazi mema au nyumba nzuri na  
maisha yenye raha na furaha. Haya yanathibitishwa katika wimbo wa Kiswahili wa  
**Mister Mahmoud:**

**Nakushukuru mpenzi kwako kuipata jaha**

**Kunipa mema makazi na maisha yenye raha**

##### **2.3.4.2 Kushauriana na Kuelekezana**

Kwa kuwa mwanamume ndiye kiongozi wa familia, alitarajiwa kumshauri,  
kumwelekeza na kumfunza bibi harusi maadili mema katika jamii yao. Bibi harusi

anamchukulia mumewe kama mwalimu mwenye makini na uhodari mkubwa na pia ambaye amehitim. Haya yanadhihirisha heshima ambayo bibi harusi anamwonyesha mumewe. Hatimaye , bibi harusi anampenda mumewe zaidi kwa sababu ya kuwa ni mume anayewajibika. Haya yanadhihirishwa na wimbo wa **Mister Mahmoud**.

**Kwa hakika ni mwalimu mwenye makini kufunza  
Hodari uliohitimu mambo yako miujiza.**

#### **2.3.4.3 Majukumu ya Nyumbani**

Nyimbo za harusi za Kiswahili zinawaelekeza maarusi katika majukumu mbalimbali ya nyumbani. Katika wimbo wa **Qasida za Harusi (Hamisa Obeid)** maarusi wanashauriwa kwamba kwa radhi za Mwenyezi Mungu maarusi wanalo jukumu la kuwapata na kuwalea watato wenyewe fahamu nzuri.

**Kwa radhi za mtume  
Waishi kufanya mema  
Na watoto wao Mola awajalie  
Fahamu nzuri uwabariki**

Katika wimbo wa Mister Mahmoud, bwana harusi anaambiwa kuwa ni jukumu lake kumpa mkewe makazi mema na maisha yenyeye raha. Anaendelea kuambiwa kuwa kwa hakika, yeye ni mwalimu mwenye makini katika kumtunza mkewe .Hivyo basi ni jukumu la bwana harusi kumpa bibiye mwelekeo mwema na kumtunza katika mambo mengi katika maisha yao ya ndoa. Bibi harusi anamshukuru bwana harusi kwa kumpa makazi mema na kumwonyesha mapenzi ya hali ya juu. Bibi harusi anaposema kwa mumewe ni mwalimu mwenye makini na kuwa hana asilolifahamu na kwamba kila mchezo anajua kucheza , anaamisha kuwa mumewe anashiriki ngono vizuri sana

**Nashukuru mpenzi kwako kuipata jaha  
Kunipa mema makazi na maisha yenyeye raha  
Kuijenga yangu enzi kwa pendo lenye furaha**

**Kwa hakika ni mwalimu mwenye makini kufunza  
Hodari alohitimu mambo yako muijiza  
Huna usilofahamu kila mtezo wateza**

Katika wimbo wa **Tupendane Wabaya Waulizane**, majukumu kadhaa ya maarusi yanetajwa, kama vile:-

- Bibi harusi kumbeba mumewe na kumpeleka kuoga , kumlisha chakula hadi ashibe vizuri
- Bibi kumbembeleza mume hadi usingizi umparamie
- Wote wawili kujaliana
- Bibi kumpikia mume chai yenyе tangawizi nyingi na kumtayarishia maji ya parachichi.

Mfano katika wimbo:-

**Honey, nataka nibebe unipeleke kuoga  
Sweetie unilishe nishibe hata mlo uso mboga  
Kisha unipe kila kitu tulichohalalishiwa.**

**Sweety usiku unibembeleze uje mwema usingizi  
Unijali nikujali vipembeni wanong'one  
Honey, basi nipe chai yenyе nyingi tangawizi  
Kisha nitayarishie juizi ya parachichi**

### **2.3.5. Mapenzi**

Katika wimbo wa **Kheri Ishallah**, maarusi wana jukumu la kuishi milele yote katika mapenzi kwani mapenzi yao ndiyo yalipelekea kuoana kwao. Sheria za Kiislamu zinawahitaji kuishi kwa mapenzi katika ndoa yao.

Maarusi wanatarajiwa kupendana, kwani upendo ndio mhimili mkuu katika ndoa. Hivyo basi , nyimbo za harusi za Waswahili zinaonyesha mapenzi kwa maarusi . Nyimbo za mapenzi huwa na maudhui au ujumbe wa kimapenzi. Sifa za nyimbo za mapenzi ni kama vile maneno matamu yenyе hisia nzito nzito, maneno yenyе kumsifu mapenzi fulani, kuutambua uhusiano mzuri na mapenziwe na kumbembeleza mapenzi miongoni mwa sifa nyinginezo. Majukumu ya nyimbo za mapenzi ni kama vile kusifu

tabia au umbo la mpenzi kwa kutaja tabia chanya na umbo zuri la mpenzi, kutakasa hisia za watu wapendanao, kupitisha maarifa au elimu ya jamii kwa kutoa mawaidha ya unyumba kwa maarusi wapya, aidha matarajio ya jamii na majukumu yao mapya kama mke na mume hupitishwa kwa nyimbo za mapenzi. Mfano wa wimbo unaothibitishia mapenzi kwa maarusi ni kama ufuatao:-

**Kheri bwana kharousi na bibi kharousi**

**Wakae hadi milele**

**Kwa sheria za Kiiislamu**

**Kheri minaall haa kheri ya kharousi**

**Kwa kweli wamependana**

**Ndio maana wakaoana**

**Menidhibiti kikweli mpenzi menizuiya**

**Umeitweka akili yangu imenipotea**

**Umeitweka akili yangu imenipotea**

**Sitoki sendi mahali kwako nimezoea**

**I love you Mr Mahmould**

**I love you Mr Mahmoud**

Katika wimbo wa **Harusi wa Issa Matona**, maudhui ya mapenzi yanajitokeza pale ambapo bibi harusi anaambiwa amrithie mumewe kwa kila analolitaka . Bibi harusi anapopelekwa kwa nyumba ya mumewe , anaambiwaacheke na mume wake na ampumbaze chumbani.

**Umrithie mumeo kwa kila analotaka**

**Unapopelekwa kwako mama unafika nyumbani**

**Ukacheke na mumeo mama**

**Umpumbaze chumbani.**

### **2.3.6 Maudhui ya Kuburudisha**

Nyimbo za Waswahili zina maudhui ya kuburudisha hadhira siku ya harusi . Nyimbo zinazoitwa ‘ Taarab’ ni mfano wa nyimbo za burudani . Maana ya ‘ Taarab’ ni ngoma ya kusisimua. Kamusi ya Kiswahili na Kiingereza ya Johnson ( 1935) anaeleza ‘ taarab’ kama mziki wa gambusi na zeze wenyewe kufuatana na mwimbaji. Neno “ taarab ‘ ni la asili ya Kiarabu lenye maana ya furaha , kusherehekeea karamu, kuimba na kupiga muziki. Mbali na neno lenyewe kuwa la kigeni, ngoma na muziki unaoambatana na taarab ni ngeni . Kwa mujibu wa Saleh ( 1980), ngoma ya ‘taarab’ hutumia ala za muziki wa Kiarabu kama gambusi (Uddi), zeze ( fidla), ganuni, dumbak na firimbi au nai. Mbali na ala hizi, ala zingine hutumika kuongeza uzito wa sauti za juu ya zile ala za misingi kwa mfano gitaa, akodiani, ogani na tarumbeta.

‘Taarab’ ni ngoma ya nyimbo na vinanda, na hakuna kucheza . Wapiga ngoma na vinanda hujikusanya mahali pamoja na wasikilizaji huwakabili au huwazingira. Ngoma ya taarab inapoanza wasikilizaji huwa kimya kabisa na jukumu lao huwa ni kutega masikio tu kwa milio ya vinanda yenye. Hadhira huwa haina la kushiriki.

Kimaudhui, nyimbo za Taarab zilipoanza zilikuwa za kusifu na kumtukuza Sultani na dhuria yake. Wakati mwingine ngoma ya taarab ilisifu na kukomaza mapenzi ya jumuiya ya Kifalme. Maudhui ya nyimbo za taarab yaweza kugawanywa katika matapo yafuatayo:- nyimbo za mapenzi , uasherati na ugoni. Katika tapo hili nyimbo nyingi huwa ni zile zinazoashiria mapenzi ya mke na mume. Katika miaka kabla ya uhuru taarab ilishughulikia zaidi nyimbo za mapenzi , kama vile mapenzi kati ya mke na mume, mapenzi ya wazee , mapenzi ya jamii, mapenzi ya kindugu na mapenzi ya nchi.

Kwa upande wa lugha, nyimbo za taarab hutumia Kiswahili cha hali ya juu, lugha ya kiishara na mafumbo . Katika muktadha wa kileo ‘taarab’ huchezwa harusini, michezoni, vilabuni mwa pombe , katika starehe za mtu binafsi au katika dhifa maalum. Katika kutamba taarab , kuna mipaka kwa vile mutribu hawezি kuongeza kitu chochote ambacho hakijafanyiwa mazoezi hapo awali . Madoido ya mwimbaji hayana nafasi wakati taarab inapoendelea. Mutribu hulazimika

kujifunga na mambo yale tu ambayo washirika wote waliyafanya mazoezi. Uhuru wake huwa katika matumizi yake ya sauti apendavyo na kuweka shada, misokoto na mikato ya maneno katika mapigo ya mahadhi ya wimbo . Washiriki katika nyimbo za taarab huwa watu wa tabaka la kati, na hadhira huwa watu wa tabaka la juu au la kati tu. Katika taarab vyombo vingi vya kimuziki hutumiwa kuchangia uwasilishaji.

Muziki wa taarab hutumiwa kwa lengo la kuburudisha kwa kuiteka na kuinyaka hadhira katika utamu, ladha na anasa za tafrija pamoja na kuzikolea hisia kwa maneno yanayoimbwa . Taarab hushirikisha wake na waume, lakini kuna uwezekano wa kuwa na waume tu au wake pekee. Dhima ya taarab ni kufunza na kuendeleza amali za jamii pamoja na falsafa yake. Taarab pia huwa na dhima ya kuburudisha , hivyo basi hutumika katika sherehe zote za jamii ikiwepo sherehe ya harusi.

Mfano wa wimbo wa taarab:-

**Heko! Mapenzi yazidi , walie , wivu wenzetu**  
**Heko! Lako lisirudi , wala lisishike kutu**  
**Heko! Kijana asadi , katika biladi zetu**  
**Ndoa aridhi mlinzi, ndoa aridhi binti.**

**Heko! Mwenye jitihadi , huwa tegemeo letu**  
**Heko! Halitasaidi , la ujana kuwa kwetu**  
**Heko! Si umaridadi , sisi si wanyama mwitu**  
**Ndoa aridhi mlinzi , ndoa aridhie binti**

Wimbo huu wa ‘taarab’ wa Amri Abedi una kusudi la kuburudisha hadhira na pia kuwapongeza maarusi katika ndoa yao.

### **2.3.7. Kufana kwa Harusi.**

Maudhui ya kufana au kufanikiwa kwa harusi yamedhihirishwa katika nyimbo za harusi za Kiswahili . Katika wimbo wa **Qasida za Harusi** mwimbaji anelezea kuwa sherehe ya harusi imeshawadia na imeshatimia, na kwamba harusi ni baraka kutoka kwa Mungu.

Mfano katika wimbo:

**Imeshawadia na imeshatimia  
Harusi ya Baraka**

Mwimbaji anaendelea kusema kuwa kuna haja ya kushangilia harusi kwani harusi ni jambo jema na lenye heri.

**Tushangilie harusi minnn Sunnaaa  
Ni jambo la kheri fiii uumaaa**

**Ndoa kwetu ni halali minn sunnnaaaa  
Ni jambo jamili ili fiii uumaa**

Katika wimbo wa **Harusi wa Issa Matona**, kufana kwa harusi kunadhihirishwa pale ambapo watu mbalimbali kama mama, dada, shangazi na somo yake bibi harusi wanaambiwa waingie uwanjani na kucheza na bibi harusi . Msanii anaendelea kumwambia bibi harusi kuwa siku hiyo ya harusi ndipo amempata mume.

**Mamaye harusi aje hapa  
Shangazi yake harusi naye nataka aje hapa  
Na dadake harusi naye nataka aje hapa  
Na bibi yake harusi naye nataka aje hapa  
Waje hapa tuhangaike naye x 4**

**Leo ni leo x 2  
Mtauona mpambano  
(Kweli si uongo ) x 3**

**Leo umepata wako mama  
Maharada wako wakome  
Waje hapa tuhangaike naye x4**

Wimbo wa **Salaam Bwana Kharousi** unadhihirisha ufanisi wa harusi pale ambapo msanii anasema kuwa anawapongeza bwana na bibi harusi , na kuwaombea mema kwani wameshatimiza jambo lenye maana kama alivyoeleza mtume.

Jambo ambalo limetimizwa hapa ni kufunga pingu za maisha.

**Kwa bwana na bibi kharousi**

**Twawaombea mema**

**Wameshatimiza jambo lenye maana**

**Alolihusia Mtume heshima**

Ni bayana kuwa maudhui ya kufana kwa harusi yamejidhihirisha vyema katika nyimbo za harusi za Waswahili.

### **Hitimisho**

Katika sura ya pili, tumefanya uchambuzi wa maudhui ya nyimbo za harusi za Wameru na za Waswahili. Tumerejelea nadharia ya uhalisia ambayo inapendekeza kazi ya fasihi iwasilishe maisha ya jamii katika mazingira ya kawaida na kuonysha ukweli wa mambo katika jamii kwani ni mambo yanayoonekana wazi katika jamii. Kwa kweli sherehe ya harusi ni jambo la kawaida na hufanyika katika mazingira ya kawaida ya wanajamii . Maudhui katika nyimbo za harusi katika jamii lengwa yanatoa taswira halisi ya maisha ya kawaida katika jamii mahususi.

Tumeweza kufafanua dhana ya maudhui na pia kuchambua maudhui kama vile kusifu maarusi na wazazi, ushauri na mawaiidha kwa maarusi, kufana kwa harusi, kuonya au kutahadharisha wahusika , kuburudisha , mapenzi, majukumu ya maarusi na mengineyo katika jamii lengwa.

## **SURA YA TATU**

### **FANI KATIKA NYIMBO ZA HARUSI ZA KIMERU NA KISWAHILI**

#### **3.0 Utangulizi**

Katika sura hii, tumeshughulikia fani katika nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili. Tumefafanua dhana ya fani tukirejelea maoni au fafanuzi za baadhi ya wasomi. Pia tumejikita katika kuchunguza aina mbalimbali za tamathali za usemi ambazo zimetumiwa katika nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili kwa jumla, huku tukieleza maana zake

Baada ya kufanya hivyo, tumechunguza baadhi ya tamathali ambazo zimetumika katika nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili. Tumejikita katika nadharia ya Leech ( 1969) ya umitindo, ambao wataalamu wengi, kama tulivyoelezea katika sura ya kwanza, wanashikilia kuwa mtindo unaakisi njia ya mwandishi au msanii ya kuwasilisha ujumbe wake kwa msomaji.

Tumeshughulikia vipengele kadhaa vya kifani kama vile toni, matumizi ya lugha, uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, takiriri, maswala ya balagha na vipengele vinginevyo . Tumefanya uchambuzi wa jinsi ambavyo msanii au mwimbaji ametumia vipengele hivi vya kifani katika kuwasilisha kwa kikamilifu ujumbe wake katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili.

#### **3.1 Fani katika Nyimbo za Harusi za Kimeru**

Nyimbo za harusi za Kimeru zimetumia baadhi ya fani katika kuwasilisha maudhui mbalimbali kwa maarusi, wazazi au jamii kwa jumla.

##### **3.1.1 Toni**

Nyimbo za harusi zinaweza kuwa na toni ya furaha, huzuni, kejeli, mapenzi au msisitizo kutegemea ujumbe unaowasilishwa na msanii. Kwa mujibu wa Wamitila, ( 2003), toni ni mabadiliko ya sauti katika neno moja yenyе kuleta mabadiliko ya maana. Toni ni mseto au mchanganyika wa hisia zinazowasilishwa na mhusika au hisia zinazowasilishwa na mhusika au mwimbaji, kama vile toni ya furaha , huzuni, kejeli, msisimko, mapenzi na kadhalika.

### **3.1.1.1 Toni ya Furaha**

Toni ya furaha katika nyimbo hujitokeza katika nyakati mbalimbali. Wakati wa asubuhi ambapo jamii ya bwana harusi huwasili nyumbani kwa bibi harusi ili kumchukua bibi harusi wampeleke kanisani, watu huimba kwa furaha kubwa. Baada ya ibada ya kufunga pingu za maisha, watu huimba kwa shangwe na vigelegele, hasa wakati maarusi wanavishana pete, kupigana busu na kutia sahihi katika cheti rasmi cha ndoa. Toni ya furaha pia hushuhudiwa wakati wa sherehe hasa maarusi wanapokata na kulishana keki, wakati wa nyimbo za tumbuizo au burudani hasa watu wanapopokea vyakula na baada ya kufana kwa sherehe ya harusi.

Mfano wa wimbo:-

**Kiongozi** : **Gikubwa ii ii**

**Wote** : **Gikubwa ii gikubwa kiatho**

**Kiongozi** : **Muiki ena mbete gikubwa ii ii**

**Wote** : **Gikubwa ii ii gikubwa ii ii**

**Gikubwa kiatho**

### **Tafsiri**

**Kiongozi** : **Imefana ee ee**

**Wote** : **Imefana harusi**

**Kiongozi** : **Bibi harusi amevikwa pete ii imefana harusi**

**Wote** : **Imefana harusi**

### **3.1.1.2 Toni ya Huzuni**

Toni ya huzuni hujidhihirisha wakati ambapo wanajamii hawana furaha siku ya harusi. Kwa mfano, wazazi wa bibi harusi wanapomtoa bibi harusi nyumbani ili apelekwe kanisani, wakati wa ibada ya harusi wazazi wa bibi harusi wanapomkabidhi mwana wao kwa wazazi wa bwana harusi na pia baada ya sherehe ya harusi wakati jamii ya bibi harusi wanaenda nyumbani na kumwacha mwana wao ugenini. Toni ya huzuni pia hujitokeza wakati bibi harusi anaposindikizwa kwa nyumba ya kwa bwana harusi katika wimbo wa **mbirira muthoni**, jamii ya bwana harusi hudhihirisha toni ya huzuni wanapoomba msamaha kwa sababu ya kuchelewa.

Mfano katika wimbo:-

**Mpumite , karaja ntiguceri**

**Mucii jwa muthoni ntigucereri**

### **3.1.1.3 Toni ya kukejeli**

Mwimbaji anatumia toni yenyeye maneno ya kukejeli au maneno ya dharau na kufanya mzaha.

**Mfano katika wimbo:-**

**Mwana ti mbetiri atuura ngarine**

**Mwana ti mbetiri atura ngarine**

**Mwana ti ncaabi araara gwakirua**

**Mwana ti ncaabi araara gwakirua**

### **Tafsiri**

**Mtoto si betri aishi kwa gari**

**Mtoto si betri aishi kwa gari**

**Mtoto si maharagwe apikwe usiku kucha**

**Mtoto si maharagwe apikwe usiku kucha**

### **3.1.2 Matumizi ya Tamathali za Usemi**

Tamathali za usemi ni fungu la maneno lililogeuzwa maana yake kamili ili kuwakilisha maana nyingine . Humwezesha msanii kuyasema anayoyataka kwa njia inayoacha athari kwenye sikio la msomaji au msikilizaji.

Nyimbo za harusi za Kimeru hutumia baadhi ya tamathali za usemi kwa kusudi la kuwasilisha ujumbe au maudhui mbalimbali.

### **3.1.2.1 Tamathali za Mafumbo**

Haya ni matumizi ya mafumbo kama dhihaka, tasfida, stihizai, kejeli au kinaya kwa kusudi la kuficha au kufumbata maana.

Kwa mfano, tasfida ni maelezo yanayolenga kupunguza makali ya maneno kwa kuficha ubaya ili kuepukana na aibu.

Mfano katika wimbo:-

**Mbirira ngino nthaka arête rubunguro**

**Nyomba e mutana ikwona muruguri**

### **Tafsiri**

**Mwambie mama mkwe alete ufunguo**

**Nyumba ya mwanawe imepata wa kufungua**

Ujumbe unaowasilishwa kwa mamake bwana harusi ni kuwa tangu siku hiyo ya harusi, bibi harusi ndiye mwenya nyumba, hivyo basi, mama mkwe asidhubutu kuingia bila hisani au ruhusa kutoka kwa bibi harusi. Ni jambo la kawaida kwa bwana na bibi harusi kushiriki ngono katika nyumba yao. Hata hivyo , ngono haitekelezwi wazi, kwani ni kitendo chenye aibu na hakistahili kutendwa wazi. Hivyo basi , mama yake bwana harusi anatahadharishwa dhidi ya kuingia kwenye nyumba ya bwana harusi , kwa kuambiwa kuwa nyumba imepata wa kufungua (mwenyeji).

#### **3.1.2.2 Tamathali za Mlinganisho**

Tamathali za mlinganisho ni kama vile sitiari, tashbiha, tashihisi au taashira. Dhana hizi hukusudia kutoa mlinganisho.

Kwa mfano, sitiari ni maelezo yanayolinganisha na kuhusisha vitu vilivyo tofauti kitabia na kimaumbile. Maana na hisia za kitu kimoja huhamishwa kwenye kitu kingine.

mfano katika wimbo wa **mwana ti mutunda**

**Mwana ii mutunda**

**Mutunda ii ui kajurimairwa**

### **Tafsiri**

**Mtoto ni mti (wa matunda)**

**Mti wa matunda hupaliliwa.**

Ujumbe unaowasilishwa katika sitiari hii ni kuwa mtoto anafananishwa na mti ambao huzaa matunda. Ili mti huo uzae mazao mema, lazima upaliliwe, utiliwe mbolea na

maji kwa wakati ufaao ili usikauke. Vile vile, msichana anapozaliwa, lazima apewe malezi mema kama vile chakula bora chenye afya, kutunzwa na kuishi vyema, na pia kupata elimu bora. Mwishowe, huyo msichana atakuwa mrembo wa kuwavutia wanaume ili wamuoe.

Usemi wa tashihisi pia umetumika katika nyimbo za harusi za Kimeru. Tashihisi ni maelezo ambayo hukipa kitu au mnyama sifa za binadamu. Katika wimbo uliopo hapo juu wa **Mwana ii mutunda**, mti wa matunda umefananishwa na msichana kwa kupewa sifa za kibinadamu.

### **3.1.2.3 Tamathali za Msisitizo**

Haya ni matumizi ya msisitizo au hali ya kutia mkazo katika maelezo au habari ili kuonyesha jinsi jambo lenyewe lilivyo muhimu. Ni dhana ya kutia chumvi au kutia chuku katika maelezo.

Mfano katika wimbo:-

**Onagwe ngino nthaka**  
**Ukanywa ‘obatini ya milo’**  
**Gikubwa ii gikubwa kiatho.**  
**Urugiri ni muko mutana**  
**Gikubwa ii ii gikubwa kiatho.**

### **Tafsiri**

**Hata wewe mamake bwana harusi**  
**Utapikiwa chai ya milo na bibi harusi**  
**Harusi imefana sana**

Wimbo huu unasisitiza jinsi ambavyo bibi harusi atamfaa mama mkwe. Bibi harusi atampikia mama mkwe chai ya ‘Ovatin’ na ‘Milo’ ambavyo ni vinywajji vitamu sana na vinavyonunuliwa kwa bei ghali sana. Huku ni kusisitiza umuhimu na ufaafu wa bibi harusi kwa wanajamii wa bwana harusi.

Katika wimbo wa **Kinanda Igikuchue**, Tamathali ya msisitizo imetumiwa wakati ambapo msanii anasema kinanda kichezwe katika hali mbalimabli , kama vile kichezewe juu, chini , tumboni , mgongoni na kadhalika , kwa kusudi la kusisitiza

furaha iliyowajaa hadhira na wachezaji wa wimbo kwa sababu ya harusi iliyofana sana.

Mfano katika wimbo:-

**Iriri riri nandi x2**  
**Kinanda igikuchue**  
**Gikuchiirwe iguru**  
**Gikuchirwe mugongo**  
**Gikuchirwe kauna**  
**Kienda gutwika gitwike**  
**Muthaka agure kingi**

### **Tafsiri**

**Leo ni leo**  
**Kinanda kichezwe**  
**Kichezewe mgongoni**  
**Kichezewe kiunoni**  
**Kikikatika bwana harusi atanunua kingine.**

### **3.1.3 Takriri**

Takriri ni urudiaji wa sauti, maneno, sentensi au vifungu kwa kusudi la kusisitiza. Katika wimbo wa harusi wa **gikubwa kiatho**, kiitikio kimerudiwarudiwa katika kila ubeti au kifungu kwa kusudi la mwimbaji kusisitiza ufanisi wa sherehe ya harusi. Hii ni aina ya takriri sentensi , kwa kuwa sentensi nzima inarudiwa.

Mfano katika wimbo:-

**Gikubwa ii gikubwa ii**  
**Gikubwa kiatho**

### **Tafsiri**

**Harusi imefana sana, harusi imefana sana**  
**Harusi imefana sana**

Takriri pia imetumika katika wimbo wa **Mwana Ii Mutunda**, kusisitiza kauli ya kumfananisha mtoto na mti unaozaa matunda, na kwamba ili mti uzae matunda bora,

unahitaji kupaliliwa. Vivyo hivyo, lazima mtoto atunzwe na apewe malezi yanayopasa ili awe mtu mzuri na anayewapendeza wanajamii. Hii pia ni takriri sentensi.

**Mwama ii mutundu**

**Mutundu ii ui kajurimairwa.**

### **Tafsiri**

**Mtoto ni mti ( wa matunda)**

**Mti wa matunda hupaliliwa**

### **3.1.4 Kubadilisha na Kuchanganya Ndimi**

Kama vile tumeelezea hapo juu, hii ni dhana ya kutumia lugha mbili pamoja zikichanganywa au kubadilishana kauli na kutumiwa kwa zamu. Dhana hii hajitokezi sana katika nyimbo za Kimeru. Hata hivyo, Wameru hutumia maneno machache ya lugha ya Kiingereza na kuyaingiza katika lugha ya Kimeru. Kwa mfano, katika wimbo wa **kaana ni keega** neno la Kiingereza ‘mobile (simu ya mkono au rununu) limetumiwa

Mfano katika wimbo:-

**Ncurubi iretiire mwerine**

**Ireja na ‘mobile’ twaragia Amerika**

### **Tafsiri**

Rika la ‘**Ncurubi**’ walienda mwezini

**Wakaleta rununu / simu ya mkono**

Ndio tuweze kuwasiliana hadi Marekani.

### **3.1.5 Utahozi**

Hii ni hali ya kukopa maneno kutoka lugha moja na kuyaingiza katika lugha nyingine kwa kulipa matamshi na maendelezo yanayowiana na lugha hiyo pokezi huku maana yake ikidumishwa. Katika wimbo wa **Mbirira Muthoni** neno la Kiingereza ‘boutique’ (nguo mpya kutoka jumba la kuuza nguo) limetoholewa na kuingizwa katika lugha ya Kimeru na kuandikwa kama ‘mbotiki’

Mfano katika wimbo:-

**Mbirira muthoni ntigucereri**

**Ni ‘mbotiki’ ngwikaira ibungo**

**Tafsiri**

**Waambie wazazi wa bibi harusi sikutarajia kuchelewa**

**Nilikuwa nashona vifungo kwenye nguo ya harusi.**

Katika wimbo wa **Gikubwa kiatho** neno ‘ovitin’ (kinywaji kama vile Milo) limetoholewa na kuwa obatini’, neno ‘suit’ limetoholewa na kuwa ‘cuti’ (vazi la kiume)

Mfano katika wimbo:-

**Onagwe ngino nthaka ukanywa ‘Obatini’ ya Milo**

**Gikubwa kiatho**

**Na ‘cuti’ ya muthaka nigwe ukauraga**

**Gikubwa ii gikubwa kiatho.**

Katika wimbo mwana ti mbetiri neno la Kiingereza ‘battery’ limetoholewa na kuingizwa katika lugha ya Kimeru na kuwa ‘mbetiri’

Mfano katika wimbo:-

**Mwana ti ‘mbetiri’ atuura ngarine**

**Mwana ti ‘mbetiri atuura ngarine**

Katika wimbo wa **Kinanda Igikuchwe** neno ‘net’ la Kiingereza limetoholewa na kuingizwa katika lugha ya Kimeru na kuendelezwa kama ‘neti’.

Mfano katika wimbo:-

**Iriri riri nandi Iriri riri nandi**

**Muiki wina neti**

**Kinanda igikuchwe**

**Tafsiri**

**Leo ni leo**

**Bibi harusi mwenye neti tunaye**

### **3.2 Fani katika Nyimbo za Harusi za Kiswahili**

Nyimbo za harusi za Waswahili zimetumia baadhi ya fani katika uwasilishaji wa maudhui mbalimbali kwa maarusi, wazazi au jamii kwa jumla.

#### **3.2.1 Toni**

Kama vile tumefafanua hapo juu, katika uchunguzi wa matumizi ya toni katika nyimbo za harusi za Kimeru, ni dhahiri kuwa nyimbo za harusi za Kiswahili pia hutumia toni mbalimbali katika kuwasilisha ujumbe.

##### **3.2.1.1 Toni ya Furaha**

Katika wimbo wa **Qasida za Harusi wa Hamisa** Obeid, waimbaji, ambao ni wanaume wanatumia toni ya furaha katika kuwasilisha ujumbe wao. Wanashangilia kuwa siku ya harusi imewadia na harusi ni jambo jema na la heri hasa katika jamii.

Mfano katika wimbo:-

**Tushangilie harusi minnn sunnaaa**

**Ni jambo la kheri fiii uumaa**

Katika wimbo wa **Harusi wa Issa Matona**, toni ya furaha inaepatikana pale ambapo msanii amejawa na furaha na kumpa hongera bibi harusi, huku akiwaita watu kama mama, dada, shangazi na somo yake bibi harusi, ili waingie uwanjani wacheza na kuifurahi pamoja na nini harusi.

**Hongera mwanangu**

**Hongera Mwanangu**

**Sisi wazazi twasema yu wapi**

**Wapi mama harusi**

**Aje hapa**

**Tuhangaike naye x 2**

**Shangazi yake harusi nataka aje hapa**

**Dadake harusi nataka aje hapa**

**Bibi yake harusi nataka aje hapa.**

**Somo yake harusi nataka aje hapa**  
**Waje hapa**  
**Tuhangaike naye x4**

### **3.2.1.2 Toni ya Unyenyekevu**

Toni ya unyenyekevu hudhihirisha heshima na utiifu kwa madhumuni ya kupata kitu fulani. Katika wimbo wa **Mister Mahmoud** toni ya unyenyekevu inajidhihirisha, ambapo mpenzi mmoja anamshukuru mwingine kwa kumuo, kumpa makazi mema na maisha yenyeye raha na vile vile, kumwonyesha mapenzi ya dhati.

Mfano katika wimbo:-

**Nashukuru mpenzi kwako kupata jaha**  
**Kunipa mema makazi na maisha yenyeye raha**  
**Kunipa mema makazi na maisha yenyeye raha**  
**Kuijenga yangu enzi kwa pendo lenye furaha.**

Katika wimbo wa **Tupendane wabaya Waulizane**, toni ya unyenyekevu pia inadhihirishwa wakati wapenzi wawili anaahidiana kila mmoja amnyenyekiee mwensiwe

Mfano katika wimbo:-

**Tupendane kwelikweli wabaya waulizane**  
**unijali nikujali vipembeni wanong'one.**

Katika wimbo wa **Usiche** toni ya unyenyekevu imedhihirishwa pale ambapo bibi harusi anashauriwa kuwa bwana akitaka (kushiriki ngono) tafadhali ampe bila pingamizi.

Mfano katika wimbo:-

**Usiche bibi harusi usiche**  
**Bwana akitaka tafadhari mpe**

### **3.2.1.3 Toni ya Mapenzi**

Katika wimbo wa **Mister Mahmoud**, toni ya mapenzi inajitokeza , ambapo mpenzi anazidi kumweleza mpenzi mwenziwe jinsi anavyompenda .

Mfano katika wimbo:-

**I love you Mr. Mahmoud**

**I love you Mr. Mahmoud**

### **Tafsiri**

**Nakupenda Bwana Mahmoud**

**Nakupenda Bwana Mahmoud.**

Wimbo wa **Tupendane wabaya waulizane** pia unadhihirisha toni ya mapenzi.

Mfano katika wimbo:-

**Tupendane kizunguzungu kwa matamu na machungu**

**Oh! Mpenzi wangu, wabaya wetu macho wameyakondoa**

**Oh ! tuzidi kuomba Mungu penzi letu lizidi kuendela.**

**Tupendane kwelikweli wabaya waulizane**

**Liwaume penzi hili vipembeni wanong'one**

**Wawili wakipendana adui hana nafasi**

**pendo tumelizingwa kwa yasini tatu.**

**Lisije kuhusudiwa na macho ya watu.**

### **3.2.2 Matumizi ya Tamathali za Usemi**

Nyimbo za harusi za Kiswahili imetumia baadhi ya tamathali za usemi kwa kusudi la kuwasilisha maudhui mbalimbali.

#### **3.2.2.1 Tamathali za Mafumbo**

Mwimbaji ametumia mafumbo, yaani lugha ambayo ni fiche, ili maana yake isieleweke waziwazi. Katika wimbo wa **Tupendane wabaya waulizane**, tamathali ya mafumbo imetumiwa.

Mfano katika wimbo:-

**Wazushi tuwaringie**

**Timu yetu kali kwa mechii**

**Timu yetu kali kwa mechii**

Huu ni ujumbe fiche kwani hakuna timu zinazocheza mechii. Ujumbe fiche ni kuwa wapenzi hao wawili wanayatekeleza mambo yao kwa uhodari sana, kiasi cha kulinganishwa na timu inayocheza mechii vizuri sana.

Katika wimbo wa **Usiche** lugha ya mafumbo imetumiwa ambapo bibi harusi anaambiwa kwamba bwana harusi akitaka tafadhali ampe. Ingawa mwimbaji hajataja ni nini ambacho kinazungumziwa, ujumbe uliofumbwa na maana yake ya wazi ni kushiriki ngono au mapenzi.

Mfano katika wimbo:-

**Usiche bibi harusi usiche**

**Usiche bibi harusi usiche**

**Usiche bibi harusi usiche**

**Bwana akitaka tafadhali mpe.**

Katika wimbo **Usiche** lugha ya mafumbo imetumiwa ambapo bwana harusi anaambiwa asiogope, kwani ametoa pesa kununua chake. Kinachorejelewa hapa ni kwamba bwana harusi ametoa mahari ili amuoibibiye.

Mfano katika wimbo:-

**Usiche bwana harusi usiche**

**Umetoa pesa kununua chako**

**Usiche bwana harusi usiche.**

Katika wimbo wa **Mister Mahmoud** lugha yenyeye mafumbo imetumiwa ambapo bibi harusi anamsifu bwana harusi kwa kusema kuwa yeye ni mwalimu mwenye umakinifu anapofunza na kwamba uhodari wake ni wa hali ya juu sana. Bibi harusi anaendelea kueleza kwamba bwana harusi anayafahamu mambo yote, na kila atendapo jambo, hilitenda kimiujiza au kwa njia hasa isiyoleweka. Ujumbe unaorejelewa hapa umefumbatwa, kwani bwana harusi si mwalimu. Kinachorejelewa

ni kuwa bwana harusi ni mume anayetekeleza mambo yote ya unyumba kwa umakinifu sana na hakuna jambo asilolijua.

**Kwa hakika ni Mwalimu mwenye makini kufunza**  
**Hodari ulohitimu mambo yako miujiza**  
**Hodari ulohitimu mambo yako miujiza**  
**Huna usilofahamu kila mtezo wateza**

Tamathali za mafumbo pia ni mbinu ambayo imetumiwa katika wimbo wa Tupendane wabaya waulizane.

Mfano katika wimbo:-

**Sweetie unilishe hata mlo uso mboga**  
**Kisha unipe kila kitu tulichochaha lalishiwa**  
**Nami nikupe mavitu we mwenyewe unaniju**  
**Kisha tucheze sebende letu mpaka joto analia.**

**Unavyocheza sebende I love you darling**  
**Ah! Habiti wangu usipunguze dozi, mimi bado sijapoa**  
**Daktari wangu dawa zako we ndo zitonisaidia.**

Ujumbe uliofumbatawa katika mafumbo ni kuhusu kushiriki ngono kwa hawa wapenzi wawili

### **3.2.2.2 Tamathali za Msisitizo**

Kama vile tumeelezea hapo juu, hii ni hali ya kutia mkazo katika maeleo ili kuonyesha jinsi jambo lenyewe lilivyo muhimu. Hii ni hali ya kutia chuku au kutia chumvi. Katika wimbo wa **Tupendane wabaya waulizane**, tamathali ya msisitizo imetumiwa ili kusistiza mapenzi ya wawili wapendanao. Msisitizo huu unanuia kuonyesha kiwango cha juu sana cha mapenzi ya bwana na bibi harusi, mapenzi ambayo hayawezi yakavunjwa na mahasidi

Mfano katika wimbo:-

**Tupendane kizunguzungu kwa matamu na machungu,  
Oh! Mpenzi wangu , wabaya wetu macho wameyakondoa  
Oh! Tuzidi kuomba Mungu , penzi letu lizidi kuendelea  
Tupendane kwelikweli wabaya waulizane.**

Katika wimbo wa **Harusi wa Issa Matona** mbinu ya tamathali ya msisitizo imetumiwa ambapo msanii anatia chuku katika hali ya kufurahia bibi harusi kwa kuwaita watu mbalimbali ili waje wahangaike na bibi harusi, yaani wafurahi pamoja na bibi harusi

Mfano katika wimbo:-

**Mamaye harusi aje hapa  
Tuhangaike naye  
Shangazi lake harusi naye nataka aje hapa  
Tuhangaike naye  
Na bibi yake harusi naye nataka aje hapa  
Tuhangaike naye  
Na somo yake harusi naye nataka  
Tuhangaike naye.**

Mwimbaji ameendelea kusisitiza hali ya mapenzi ambapo bibi harusi anasema kuwa ameridhishwa na mapenzi ya Bwana Mahmoud, ambayo yameichukua akili yake kabisa kwamba hana lingine la kufikiria au la kufanya. Huu ni msisitizo wa mapenzi kati ya bwana na bibi harusi.

Mfano katika wimbo:-

**Menidhibiti kikweli mpenzi menizuiya  
Umenitweka akili yangu imepotea  
Umenitweka akili yangu imepotea  
Sitoki sendi mahali kwako nimeshazoea**

Bibi harusi anaendelea kusositiza kuwa usiku halali na mchana kutwa pia halali tena, kwani huwa anayawazia mapenzi ya Bwana Mahmoud. Kwa kweli, mapenzi ambayo yanamkosesha mtu usingizi ni mapenzi makubwa sana.

### **3.2.3 Takriri**

Takriri ni urudiaji wa sauti, neno au mstari fulani kwa kusudi la kusositiza. Nyimbo za harusi za Kiswahili zimetumia takriri kwa lengo la kusositiza ujumbe fulani. Katika **Qasida za Harusi za Hamisa Obeid**, kiitikio kimerudiwarudiwa baada ya kila kifungu kwa kusudi la kusositiza kuwa harusi ni sherehe iliyobarikiwa na Mungu. Hii ni takriri sentensi.

#### **Imeshawadiaa na imeshatimiaa**

#### **Harusi ya barakaaa**

Katika wimbo wa **Mister Mahmoud** kiitikio pia kimerudiwarudiwa kwa kusudi la bibi harusi kusositiza mapenzi yake ya dhati kwa Bwana Mahmoud. Hii ni takriri kifungu.

**I love you Mr Mahmoud**

**I love you Mr Mahmoud**

#### **Tafsiri**

**Nakupenda bwana Mahmoud**

**Nakupenda Bwana Mahmoud**

Katika wimbo wa **Usiche**, takriri ya mstari imetumika ili kuwasitisizia maarusi kwamba wasiogope katika maisha yao mapya ya unyumba. Takriri kifungu imetumiwa kwani maneno wamerudiwa katika kifungu Kizima.

**Usiche bwana harusi usiche**

**Usiche bwana harusi usiche.**

**Ushe bwana harusi usiche**

**Ukiona bahari utaogelea**

### **3.2.4 Kubadilisha na Kuchanganya Ndimi**

Mbinu ya kubadilisha na kuchanganya ndimi au msimbo imetumiwa katika nyimbo za harusi za Kiswahili. Sababu ambazo zimechangia matumizi ya mbinu hii ni pamoja na kuwa waimbaji wana elimu na ujuzi wa lugha zaidi ya moja, ni vijana na vile vile wana lengo la kusositiza ujumbe.

Katika **Qasida za Harusi**, maneno ya lugha ya Kiarabu wametumika kusositiza kuwa harusi ni jambo jema na lilokubalika kwa Mungu na katika jamii kwa jumla.

Tushangilie harusi **minnn sunnaaa**

Ni jambo la kheri **fiii uuumaaa**

Katika wimbo wa Mister Mahmoud, msanii ametumia lugha ya Kiswahili na ya Kingereza

Mfano

**Helo, helo, helo I love you Mr Mahmoud**

**Helo, helo, helo I love you Mr Mahmoud**

**Tafsiri**

**Helo, helo, helo**

**Nakupenda Bwana Mahoud**

**Usiku huwaza sana kukicha silali tena**

**I love you Mr Mahmoud**

Maneno yenyе asili ya Kiarabu pia yametumika katika nyimbo za harusi za Kiswahili, kwa mfano ‘Kheri’, ‘Jamili’, ‘radhi’

Katika wimbo wa **Tupendane wabaya Waulizane**,

maneno ya Kiingereza yametumiwa,

Kwa mfano:-

**Honey, sweetie ,**

**I love you darling.**

### **3.2.5 Maswali ya Balagha**

Katika wimbo wa **Harusi wa Issa Matona**, msanii ameyauliza maswali ambayo hayahitaji majibu yoyote, ila tu kuchochea fikira za hadhira.

**Sisi wazazi asema yu wapi?**

**Wapi mama harusi aje hapa tuliangaike naye.**

Katika wimbo wa **Tupendane Wabaya Waulizane**, swali la balagha limeulizwa ambapo msani anasemi ni nini ambacho watu wataulizana . Swali ambalo watu wataulizana ni kuhusu mapenzi ya wawili waliopendana.

**Mfano katika mfano:-**

**Tupendane kwellikweli wabaya waulizana**

**Unijali nikujali vipembeni wanong'one**

Haya ni maswali ambayo hayahitaji kujibiwa . Katika wimbo wa **Salaam Bwana Kharousi** maswali ambayo yameulizwa hayahitaji majibu ya moja kwa moja  
Mfano katika wimbo:-

**Ewe ndugu yangu wasubiri nini ?**

**Jambo la kuoa utafanya nini”**

### **3.2.6 Kufupisha na Kurefusha Maneno.**

Mbinu ya kufupisha na kurefusha maneno hutumiwa sana katika ushairi, ambapo lengo huwa ni utoshelezi wa mizani na vina katika shairi. Mbinu hii imetumika katika nyimbo za harusi za Kiswahili, ambapo baadhi ya maneno yamefupishwa au kurefushwa ili kutosheleza mahadhi au mapigo katika wimbo.

Katika wimbo wa **Mister Mahmoud**, mbinu ya kufupisha na kurefusha maneno imejidhihirisha.

Mfano:

**Kufupisha maneno**

**Menidhibiti**

**Menizuiya**

**Sendi**

**Kiwa**

**Unipayo**

**Kateremsha**

**Ulohitimu**

**Usilofahamu**

**Kawaida (Kiswahili sanifu)**

**Umenidhibiti**

**Umenizuia**

**Siendi**

**Nikiwa**

**Unayonipa**

**Nikateremsha**

**Uliyohitimu**

**Usilolifahamu**

**Kurefusha maneno**

**Kawaida (Kiswahili sanifu)**

**Menizuiya**

**Umenizuia.**

**Wimbo wa Tupendane wabaya waulizane**

**Kufupisha maneno**

**Nami**

**We mwenyewe**

**Tazimia**

**Wanong'one**

**Kawaida**

**Na mimi**

**wewe mwenyewe**

**atazima**

**Wanang'onezana**

**Hitimisho**

Katika sura hii ya tatu tumejikita katika uchambuzi wa fani mbalimbali anbazo zimetumiwa katika nyimbo za haruzi za Kimeru na za Kiswahili . Tumefafanua dhana ya fani na kuchambua baadhi ya fani kama vile toni , tamathali za usemi , takrir , kubadilisha na kuchanganya ndimi na fani nyinginezo. Tumetoa mifano ya jinsi fani hizi zimetumiwa katika kuwasilisha ujumbe wa msanii, katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili.

## SURA YA NNE

### ULINGANISHAJI WA MAUDHUI NA FANI KATIKA NYIMBO ZA HARUSI ZA KIMERU NA KISWAHILI

#### 4.0 Utangulizi

Lengo kuu la utafiti wetu ni uchambuzi liganishi wa maudhui na fani katika nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili. Katika sura ya pili na ya tatu ya kazi yetu, tumefanya uchambuzi wa maudhui na fani katika nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili. Katika sura hii tumeshughulikia ulinganishaji wa maudhui na fani. Ni dhahiri kuwa kuna maudhui na fani zinazolingana na pia kutofautiana katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili.

**4.1. Ulinganishaji wa Maudhui katika Nyimbo za Harusi za Kimeru na Kiswahili**  
Kwa kurejelea maudhui katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili, ni dhahiri kwamba kuna maudhui yanayofanana au kulingana katika jamii lengwa na vile vile kuna maudhui ambayo yanatofautiana.

##### 4.1.1. Maudhui Yanayolingana

Kwa kurejelea maudhui katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili, lengo kuu la msanii ni kuwashauri au kuwapa mawaidha maarusi, wazazi wao au jamii kwa jumla.

###### 4.1.1.1 Ushauri na Mawaidha kwa Maarusi

Katika sura ya pili sehemu ya 2.2.2. tumeelezea kuwa kuna nyimbo za Kimeru zilizoimbwa katika sherehe ya harusi ili kuwashauri na kuwapa maarusi mawaidha katika maisha yao mapya ya ndoa . Wimbo wa **Garura Mithiire** ni mojawapo ya nyimbo za harusi za Kimeru, ambao unawashauri maarusi kubadilisha mienendo waliyokuwa nayo kabla ya kuolewa , na kuiga mienendo inayoendana na maisha yao mapya ya ndoa. Kwa mfano , bibi harusi anashauriwa kuwajibika katika ndoa , kwa kumtunza mume na watoto kwa kila hali, naye bwana harusi anahimizwa kumpenda bibi yake na watoto na kuhakikisha ametosheleza au kukidhi mahitaji yao yote.

Katika wimbo wa Kiswahili wa Usiche, bwana harusi anashauriwa kwamba asiogope chochote maishani. Anaendelea kushauriwa kuwa akiona bahari ataogelea hadi avuke ng'ambo nyingine. Bibi harusi naye anashauriwa kuwa asiogope chochote , na bwana harusi akitaka ampe . Huu ni ujumbe au ushauri uliofumbatwa, ili maana yake yasieleweke waziwazi . Ujumbe uliofumbatwa ni kuhusu kushiriki ngono. Hivyo basi, ni bayana kuwa maudhui ya ushauri na mawaidha kwa maarusi ni maudhui yanayolingana katika nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili. Hata hivyo , ni vizuri kuelewa kuwa mawaidha na ushauri unaweza kuwa tofauti , lakini ukweli ni kwamba ushauri unapatikana katika jamii zote mbili.

#### **4.1.1.2. Kupongeza au Kusifu Maarusi**

Katika 2.2.1 hapo juu tumeelezea kuwa kuna nyimbo za harusi za Kimeru ambazo hukusudia kuwapongeza au kuwasifu maarusi, kwa mfano wimbo wa **Kaana ni Keega**.

Wimbo huu huimbwa kuonyesha uzuri wa mtoto, hasa atakapoolewa, atawawezesha wazazi kusafiri mbali , kupata mahari, mtoto kuwatunza wazazi katika maisha yao ya uzeeni na mengineyo. Katika 2.3.3 tumeelezea kuwa nyimbo za harusi za Kiswahili pia zilikusudia kuwapongeza na kuwasifu maarusi . Katika wimbo wa **Qasida za Harusi wa Hamisi Obeid** , msanii anawaambia maarusi kwamba harusi ni njema na ni kitendo kinachofurahiwa na watu wote katika jamii. Hivyo basi, maudhui ya kupongeza au kusifu maarusi yanalingana katika nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili.

#### **4.1.1.3. Maombi au Dua.**

Katika nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili maombi au dua ni maudhui yaliyopewa kipao mbele . Katika 2.7.9 hapo juu tumeelezea kuwa harusi katika jamii ya Wameru ilichukuliwa kuwa baraka kutoka kwa Mungu. Ndiposa maombi na salae za ndoa zilisemwa wakati wa ibada ya ndoa kanisani . Nyimbo pia zinainmbwa zinazoelekeza maombi ya maarusi kwa Mungu. Katika wimbo wa **mwana ti mbetiri**,waimbaji wanasesma kuwa walikuwa wakiombea harusi ya wana wao kwa muda mrefu.

Katika 2.3.1 tumeeleza kuwa wakati wa harusi ya Waswahili kuna nyimbo amabzo zinainmbwa kwa kusudi la kuwaombea maarusi mema na baraka za Mwenyezi Mungu . Katika wimbo wa **Qasida za Harusi** waimbaji wanawaombea maarusi

dua njema kwa Mungu . Wanawaombea maarusi maisha mema yenyе kheri, na kwamba Mungu awabariki na watoto wenye fahamu nzuri . Ni dhahiri kwamba maudhui ya maombi au dua yanalingana katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili. Hata hivyo, maombi yanayoombwa kwa maarusi yanakuwa tofauti kwani maombi ya Waswahili ni ya Kiislamu ilhali maombi ya Wameru ni ya dini ya Kikristu.

#### **4.1.1.4 Kufana kwa Harusi**

Katika 2.2.3 tumeeleza kuwa nyimbo za harusi za Kimeru zina maudhui ya kushangilia na kusherehekeea ufanisi wa sherehe za harusi . Tukirejelea wimbo wa **Gikubwa Kiatho**, ni bayana kuwa wimbo huu unaimbwа kama ishara ya kufanikiwa kwa harusi . Wimbo huu uliimbwa na watu wote waliohudhuria sherehe ya harusi , wake kwa waume , wote wakidhihirisha kuridhishwa na harusi hiyo. Katika 2.3.8, wimbo wa harusi wa Kiswhaili wa **Qasida za Harusi** unaelezea kuridhika kwa waimbaji kwa kuwa sherehe ya harusi imewadia na imetimia , hivyo basi wanayo sababu ya kushangilia .

Ni bayana kuwa maudhui ya kufana kwa harusi yanalingana katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili.

#### **4.1.1.5 Kuburudisha**

Katika sehemu ya 2.2.8 hapo juu, tumefafanua kuwa nyimbo za harusi za Kimeru zilikuwa na lengo la kuburudisha hadhira, zaidi ya ya kuelezea mengine ya nyimbo.

Tumeeleza kwamba nyimbo za burudani ziliimbwa ili kuwatumbuiza watu hasa wakati wa ibada kanisani, wakati wa kupokea vyakula au wakati wa kukata keki.

Katika 2.3.7 tumeeleza kuhusu burudani katika nyimbo za harusi za Kiswhaili , hasa nyimbo za “ taarabu”, ambayo ni ngoma ya kusisimua ya Waswahili inayokusudiwa kuwatumbuiza au kuburudisha hadhira .

Maudhui ya burudani yanalingana katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili hasa tunaposhikilia maoni ya baadhi ya wasomi au wataalumu wa taaluma ya nyimbo, kuwa umuhimu mkuu wa nyimbo ni kuburudisha. Mifano ya wanataaluma hawa ni kama vile mwokozi ( 1996), Finnegan ( 1970) na wengineo.

#### **4.1.2 Maudhui Yanayotofautiana**

Katika sehemu ya 4.1.1. tumefafanua kuwa kuna maudhui ya nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili ambayo yanalingana. Katika sehemu hii tumefafanua kwa kina maudhui ambayo yanatofautiana katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili.

##### **4.1.2.1. Kuomba Msamaha**

Katika sura ya pili, sehemu ya 2.2.4, tumelezea kuwa wazazi wa jamii ya upande wa bwana harusi huomba msamaha iwapo watachelewa kufika nyumbani kwa bibi harusi ili kuomba wapewe bibi harusi wampeleke kanisani kwa ibada ya harusi . Wakati mwingine wazazi waliochelewa walitakiwa kutoa zawadi fulani kama njia ya kuomba msamaha .

Katika harusi ya Waswahili , hatujashuhudia uombaji wa msamaha katika utafiti ambao tumetekeleza . Hivyo basi maudhui haya ya uombaji wa msamaha huenda yakatofautiana katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili.

##### **4.1.2.2 Mapenzi**

Katika 2.3.5 hapo juu tumeleza kuwa lugha ya mapenzi inajidhihirisha katika nyimbo za harusi za Kiswahili . Haya ni maneno matamu yenyе hisia nzitonzo na maneno yenyе kumsifu mpenzi fulani na hasa kuibua hisia fulani za kimapenzi . Wimbo wa **Mister Mahmoud** ni mfano wa wimbo unaodhihirisha hisia za kimapenzi.

Katika utekelezaji wa utafiti wetu, hatujadhihirisha lugha ya kuibua hisia za kimapenzi katika nyimbo za harusi za Kimeru katika nyimbo ambazo tumechambua . Hivyo basi, huenda maudhui ya mapenzi yanatofautiana katika nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili.

##### **4.1.2.3 Maudhui ya Maombi au Dua**

Ingawa maudhui ya maombi na dua yanalingana katika jamii za Wameru na Washwaili tofauti iliyoko ni kwamba kama vile tumeleza hapo juu, maombi ya Waswahili yalifanywa kulingana na dini ya Kiislamu ilhali maombi ya Wameru yalifanywa kulingana na dini ya Kikristu,

#### **4.1.2.4. Maudhui ya Mawaiidha na Ushauri**

Katika ulinganishi wa maudhui ya nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili hapo juu, tumeeleza kuwa maudhui haya yamefafana. Hata hivyo , tofauti ya maudhui haya ni kuwa maudhui yalitolewa kwa njia tofauti na watu tofauti. Kwa mfano , bibi harusi katika harusi ya Waswahili alishaurirwa na kungwi, ambaye alikuwa na ujuzi na utaalamu wa ndoa na unyumba . Katika harusi ya Wameru, ushauri kwa bibi harusi ultolewa na mamake bibi harusi na wanawake wengine wa rika la mamake bibi harusi na ambao waliarikwa na mamake bibi harusi ili wamsaidie kumshauri bibi harusi . Hili ni dhihirisho kuwa maudhui ya ushauri na mawaiidha kwa maarusi yalitofautiana

### **4.2 Ulinganishaji wa fani katika Nyimbo za Harusi za Kimeru na Kiswahili**

Kwa kurejelea fani katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili , ni muhimu kuzingatia kuwa kuna fani zinazofanana, na vile vile zile ambazo zinatofautiana.

#### **4.2.1 Fani Zinazolingana**

Utafiti wetu umedhihirisha kwamba kuna fani zinazolingana katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili.

##### **4.2.1.1 Toni**

Kwa kurejelea dhana ya toni, ni dhahiri kuwa dhana hii imetumiwa katika uwasilishaji wa ujumbe katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili katika 3.5.1.1. na 3.6.1.1. Katika sura ya tatu , tumefafanua matumizi ya toni ya furaha katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili. Hivyo basi, ni dhana ambayo inalingana katika nyimbo za jamii lengwe. Aidha , ni muhimu kuzingatia kwamba toni mbalimbali zimetumika kuwasilisha ujumbe tofauti tofauti , kama vile tumeeleza katika 4.2.2. ambapo tumeelezea kuhusu fani zinazotofautiana .

##### **4.2.1.2 Matumizi ya Tamathali za Usemi**

Katika sehemu ya 3.4.2 katika sura ya tatu , tulifafanua kuwa kuna tamathali za mafumbo, tamathali za mlinganisho na tamathali za msisitizo.

Utafiti wetu umedhihirisha kuwa kuna matumizi ya tamathali za mafumbo na tamathali za msisitizo katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili .

Hivyo basi, matumizi ya tamathali za usemi ni dhana inayolingana katika jamii lengwa. Aidha ni muhimu kuzingatia kwamba utafiti wetu haukudhihirisha matumizi ya tamathali za mlinganisho katika nyimbo za harusi za Kiswahili.

#### **4.2.1.3 Takriri**

Mbinu ya urudiaji wa sauti , maneno, sentensi au vifungu kwa kusudi la kusisitiza ujumbe ni dhana ambayo inalingana katika nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili, kama inavyodhihirishwa katika 3.5.3. na 3.6.3 katika sura ya tatu. Katika wimbo wa harusi wa Kimeru wa **Gikubwa Kiatho** (3.5.3) takriri imetumiwa . Katika nyimbo za harusi za Kiswahili za **Mister Mahmoud, Usiche** na , ( 3.6.3) taKriri zimetumiwa kwa kusudi la kusisitiza ujumbe . Hivyo basi, matumizi ya takriri ni mbinu inayolingana katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili.

#### **4.2.1.4 Kubadilisha na Kuchanganya Ndimi**

Kwa kurejelea sehemu ya 3.5.4 na 3.6.4 katika sura ya tatu , mbinu ya kuchanganya na kubadilisha ndimi zimetumiwa . Hata hivyo , ufanuzi wa 3.5.4 unaonyesha kuwa dhana hii haitumiki kwa wingi katika nyimbo za harusi za Kimeru, kama inavyokuwa katika nyimbo za Kiswahili . Katika nyimbo za Kimeru, maneno machache tu, ya Kiingereza yametumiwa kama vile “ mobile’ ilhali nyimbo za Kiswahili zimetumia mbinu hizi zaidi , katika hali ya kuchanganya au kubadili ndimi kama vile tumefafanua katika 4.2.2.

Hata kama nyimbo za Kimeru zimetumia asilimia kidogo ya ubadilishaji na kuchanganya ndimi ikilinganishwa na matumizi ya dhana hii katika nyimbo za Kiswahili , ni dhahiri kuwa ni dhana zinazolingana kwa kiasi fulani katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili.

#### **4.2.2. Fani Zinazotofautiana**

Kuna baadhi ya fani zinazotofautiana katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili, kama vile tumedhihirisha katika utekelezaji wa utafiti wetu.

#### **4.2.2.1 Toni**

Katika sehemu ya 4.2.1.1 hapo juu, tumeelezea kuwa ingawa kuna ulinganishi wa dhana ya toni katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili , ni muhimu kuzingatia kuwa toni mbalimbali zimetumiwa katika kuwasilisha ujumbe tofauti tofauti, hivyo basi kuzua tofauti ya matumizi ya toni katika nyimbo lengwa . Huku toni ya furaha ikilingana katika nyimbo za Kimeru na za Kiswahili , tofauti za toni zinapatikana pale ambapo nyimbo za Kimeru zinadhihirisha toni ya huzuni ( 3.5.1.2) na toni ya kukejeli ( 3.5.1.3) ilhali nyimbo za Kiswahili zinadhihirisha toni ya unyenyeketu ( 3.6.1.2.) Haya yanadhihirisha kuwa matumizi ya toni, kwa upande mmoja yanalingana na kwa upande mwingine yanatofautiana kwa kuzingatia utafiti wetu.

#### **4.2.2.2 Tamathali za Usemi**

Katika 4.2.1.2 hapo juu, tumefafanua kuwa ingawa nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili zinalingana katika matumizi ya tamathali za mafumbo na msisitizo, tofauti inazuka pale ambapo nyimbo za Kiswahili hazijadhihirisha matumizi ya tamathali za mlinganisho kwa kurejelea utafiti wetu.

#### **4.2.2.3 Kuchanganya na Kuhamisha Ndimi**

Kwa kurejelea sehemu ya 4.2.1.4 hapo juu tumeelezea kuwa ingawa dhana hizi zinatumika katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili , tofauti inazuka pale ambapo matumizi ya dhana hii katika nyimbo za Kiswahili ni zaidi ya jinsi ambavyo zinatumika katika nyimbo za Kimeru . Huku nyimbo za Kimeru zikitumia dhana ya kuchanganya ndimi kwa asilimia kidogo sana kwa mfano katika ( Wimbo wa **Kaana ni Keega** neno la kiingereza ‘ Mobile’) nyimbo za Kiswahili zimetumia dhana hii kwa asilimia kubwa zaidi kwa mfano wimbo wa **Mister Mahmoud** ambao mbali na kuchaganya ndimi , kuna kubadilisha ndimi ( kuachilia lugha ya Kiswahili na kuingiza mistari kadhaa ya lugha ya Kiingereza Mfano katika wimbo:-

**Helo, helo , helo      I love you Mr. Mahmoud**

**Helo, helo, helo      I love you Mr. Mahmoud**

**Usiku huwaza sana kukicha silali tena**

**I love you Mr. Mahmoud**

Maelezo haya yanadhihirisha tofauti za matumizi ya kuchanganya na kubadilisha ndimi katika nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili kwa kuzingatia utafiti wetu.

#### **4.2.2.4 Utohozi**

Mbinu ya kukopa maneno kutoka lugha moja na kuyaingiza katika lugha nyingine kwa kulipa neno matamshi na maendelezo yanayowiana na lugha hiyo pokezi ni dhana inayojitokeza katika nyimbo za harusi za Kimeru, tukirejelea sehemu ya 3.5.5. katika sura ta tatu. Dhana ya utohozi haijadhihirishwa katika nyimbo za Kiswahili kwa kurejelea utafiti wetu.

#### **4.2.2.5. Kufupisha na Kurefusha Maneno**

Katika sura ya tatu sehemu ya 3.6.6. tumeelezea kuhusu mbinu ya kufupisha na kurefusha maneno katika nyimbo za harusi za Kiswahili, ambayo pia hutumika katika ushairi . Pia tumeelezea sababu za kufupisha na kurefusha maneno na kutoa mifano . Utafiti wetu haukudhihirisha dhana hii katika nyimbo za Kimeru , hivyo basi kuzua tofauti ya matumizi ya kufupisha na kurefusha maneno katika nyimbo za Kimeru na za Kiswahili ( mbinu za inkisari na mazida).

#### **Hitimisho**

Katika sura ya nne, tumeshughulikia ulinganishaji wa maudhui na fani katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili . Kusudi letu ni kuonyesha maudhui yanayolingana na kutofautiana katika nyimbo teule za Kimeru na za Kiswahili . Tumedhihirisha kuwa kuna maudhui yanayolingana kama vile ushauri kwa maarusi na wazazi, jamii kwa jumla, kupongeza au kusifu maarusi, maombi au dua , majukumu ya maarusi , kufana kwa harusi na maudhui mengineyo. Maudhui yanatofautiana ni kama vile kuomba msamaha , msisitizo wa mapenzi, kejeli na maudhui mengineyo.

Fani zinazolingana ni kama vile toni, tamathali za semi , kuchanganya na kubadilisha ndimi na takriri .

Hata hivyo kuna tofauti katika matumizi ya fani ya toni , tamathali za usemi na kuchanganya na kubadili ndimi ingawa kuna kulingana kwa fani zizo hizo.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI WA UTAFITI, CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.0 Utangulizi**

Utafiti wetu umeshughulikia uchambuzi linganishi wa maudhui na fani katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili . Lengo letu katika sura hii ni kutoa majumuisho juu ya mchakato mzima wa shughuli yetu ya utafiti . Tumeweza kujadili nadharia tete zetu pamoja na kuangazia matatizo tuliyokumbana nayo katika harakati za utafiti wetu. Pia tumetoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ambayo yatatoa mchango mkubwa kwa watafiti wengine ambao watajishughulisha na tafiti zao za baadaye.

#### **5.1 Muhtasari wa Utafiti**

Lengo kuu la utafiti wetu ni uchambuzi linganishi wa maudhui na fani katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili .

Utafiti huu umefanikiwa kujibu maswali ya nadharia tete zilizoorodheshwa kuwa kuna uhusiano na tofauti ya kimaudhui na kifani katika nyimba za harusi za Kimeru na za Kiswahili.

Ni dhahiri kuwa utanzu wa nyimbo umeshughulikiwa na baadhi ya wasomi lakini swala la ulinganishaji wa fani na maudhui katika nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili halijashughulikiwa .

Katika sura ya kwanza tumejikita katika utangulizi , tatizo la utafiti , madhumuni na nadharia tete ambazo tumehusisha katika utafiti wetu , sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, misingi ya kinadharia , yaliyoandikwa kuhusu somo la utafiti na mbinu ambazo tumetumia .

Sura ya pili imeshughulikia maudhui katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili Maudhui haya ni pamoja na kupongeza au kusifu maarusi , ushauri na mawaidha kwa maarusi na wazazi wao, maudhui ya kufana kwa harusi , maombi / dua , kutahadharisha au kuonya maarusi, kumkaribisha bibi harusi nyumbani ,

maudhui ya kuburudisha na majukumu ya maarusi miongoni mwa maudhui ambayo tumeshughulikia .

Sura ya tatu imeshughulikia matumizi ya baadhi ya fani za lugha katika uwasilishaji wa ujumbe. Fani hizi ni kama vile toni, tamathali za usemi, takriri, kubadilisha na kuchanganya ndimi na nyinginezo .

Sura ya nne imeshughulikia uchambuzi linganishi wa maudhui na fani katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili. Tumejaribu kuonyesha maudhui na fani ambazo zinalingana, na vilevile zile ambazo zinatofautiana.

Hatimaye sura ta tano imeshughulikia muhtasari wa kazi ya utafiti wetu, changamoto ambazo tumekumbana nazo katika utekelezaji wa utafiti wetu na mapendekeza ambayo huenda yakawfaa sana watafiti wa hapo baadaye .

## **5.2 Changamoto katika Utafiti wetu.**

Utafiti huu ulifanywa maktabani na nyanjani. Katika kukamilisha utafiti wetu , tulikumbana na baadhi ya changamoto . Utafiti wa nyanjani ilitugharimu sana, kwani ilitubidi tufunge safari mara kwa mara ili kukutana na wahojiwa waliotusaidia.

Harusi ni sherehe maalum sana katika jamii, hivyo basi kulikuwa na nyimbo chungu nzima tulizokusanya wakati wa utafiti wa nyanyani . Kuchuja nyimbo ambazo zinatufaa zaidi lilikuwa ni tatizo kubwa sana. Baadhi ya nyimbo hizo zilihitaji kufanyiwa tafsiri kwa lugha ya Kiswahili. Hasa nyimbo za jamii ya Waweru . Katika harakati za kutafsiri nyimbo hizo , maana ya wimbo huenda ikabadilika na vile vile kusababisha mabadiliko ya kimahadhi, hivyo basi kutoimbika kama ilivyokusudiwa.

Shughuli ya kufanya tafsiri pia ilichukua muda mrefu. Mara kwa mara, tulikumbana na wahojiwa ambao hawakuwa tayari kushirikiana kabisa na watafiti . Aidha , walihitaji kuzawadiwa kwa juhud zao, au walifikiria kuwa tulitekeleza shughuli ya utafiti ili itufaidi kifedha .

Katika jamii za Wameru na Waswahili, sherehe za harusi huandaliwa katika miezi ya Aprili, . Agosti and Desemba, hasa wakati wa likizo, ambapo shule huwa zimefungwa . Jambo hili limezua changamoto katika utafiti wetu kwani utafiti wa nyanjani uliwezekana tu kwa miezi ya Aprili na Agosti.

Muda unaotolewa kwa watafiti pia ni mchache mno, jambo ambalo linawatatiza sana katika kuutekeleza na kuukamilisha utafiti wao ipasavyo.

Kwa vyovyothe vile, tulijikakamua dhidi ya changamoto zilizotukabili, na tulifaalu katika kuutekeleza utafiti wetu.

### **5.3 Mapendekezo**

Tungependa kuwahimiza wasomi zaidi kufanya utafiti zaidi , hasa katika utanzu wa fasihi simuizi ambao unatoweka pole pole na mahala pake kuchukuliwa na fasihi andishi. Pili, maudhui na fani katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili ni eneo pana sana la kiusomi , kwa kuwa maudhui na fani hizi ni nyingi sana . Kwa kuwa tumejikita tu katika baadhi ya maudhui na fani , tungependekeza utafiti zaidi ufanywe na baadhi ya wasomi kwa lengo la kufikia yale ambayo hatukuyafikia.

## MAREJELEO

- Beja, S.K (2001), *Giriama Funeral Songs: Functional Aesthetic study*. Ph.D. Thesis, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Finnegan, R. (1970), *Oral Literature in Africa*. London: Oxford University Press.
- Hegel, G.W.F (1971), *Introduction to Aesthetics*, Oxford: Claredon.
- Johnson, F. (1935), *Kamusi ya Kiswahili*. London: Oxford University Press.
- Kinene wa Mutiso, (1985), *Hurafa na Uyakifu katika Hamziyaa*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kinoti, T.M. (2008), *Fasihi Simulizi na Utamaduni*: The Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi, Kenya.
- Kirubi, N.W. (2007), *Dhana ya Nyimbo: Sifa, Miundo, Aina Mbalimbali na Majukumu ya Nyimbo*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kitsao, J. (1975), *A stylistic Approach for the Study of Swahili Prose Texts*: Tasnifu, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Leech, G.N (1969), *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman.
- Leech, G. N & Short, M.A (1981) *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose*. London, Longman Group Limited.
- Madumulla, J.S (2009), *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.
- Matei, A.K. (2011), *Fani ya Fasihi Simulizi*. Oxford University Press..
- Mbatiah, M. (2001), *Kamusi ya Fasihi*, Standard Textbooks, Nairobi.
- Makange, J.K. (2015), *Ulinganishaji wa Fani za Kiutendi katika Nyimbo za Harusi Mionganoni mwa Jamii za Wataveta na Waswahili*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mogambi, H. (2007), *Uchambuzi wa Nyimbo za Kiswahili*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mukobwa, J.N.M. (1985), *Maudhui katika Tamthilia Tano za Ebrahim Hussein*.  
Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mbiti, J.S. (1975), *Introduction to African Religion*, Heinmann Educational Books,  
Nairobi.

Msokile, M. (1992), *Msingi wa Hadithi Fupi*. Dares Salaam; Dar es Salaam  
University Press.

\_\_\_\_\_ (1993), *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi, E.A.E.P.

Mulokozi, M.M. (1993), *Fasihi, Uandishi na Uchapishaji*. Makala ya semina ya  
umoja wa waandishi wa vitabu. Tanzania Dar es Salaam University Press &  
Wavita: Dar es Salaam.

\_\_\_\_\_ (1996), *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha  
Tanzania.

Mwai, W. (1997), *Power of Songs for the Swahili Women. In the Contesting Social  
Death: Essay on Gender and Culture*, Ed. Wanjiku K., Masinjila M. and  
Obote M.

Nairobi: Kenya Oral Literature Association.

Mboti, D. (2012), *Mtindo katika Nyimbo za Michezo ya Watoto wa Darasa la  
Kwanza, katika Tarafa ya Starehe*, Nairobi. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu  
cha Nairobi.

Mohamed, S.A. (1995), *Kunga za Nathari ya Kiswahili* East African Educational  
Publishers, Nairobi.

Ngome, M.D. (2014) *Uchambuzi wa Nyimbo za Harusi za Wadigo na Waswahili*,  
Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ngure, A. (2003), *Fasihi Simulizi ya Shule za Sekondari*, Phoenix Publishers Limited,  
Nairobi.

Ntarangwi, M. (2003) *Gender, Performance and Identity: Understanding Swahili  
Cultural Realities through Songs*, Trenton, NJ: Africa World Press.

- Njogu, K., na Chimera, R. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*: Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Ngaruthi, T.K. (2008), *Fasihi Simulizi na Utamaduni*: Nairobi, The Jomo Kenyatta Foundation.
- Nyaga, D. (1986), *Mikarire na Mituuriye ya Amiiru*. Nairobi, Heinmann Kenya.
- \_\_\_\_\_, (1997), *Customs and Traditions of the Meru*, East African. Education Publishers Limited, Nairobi.
- Odeo, I. na Maina, G. (2008), *Isimujamii kwa Shule za Sedondari*, Oxford University Press, Nairobi.
- Saleh, S.S. ( 1980), “*Nyimbo za Taarab Unguja*.” Lughu Yetu Namba 37. Jarida la BAKITA.
- Senkoro, F.E.M.K. (1987), *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press & Publicity Centre.
- Sunkuli , L. & Miruka, A. ( 1990), *A Dictionary of Oral Literature* , EAEP, Nairobi.
- Timammy, R. (2002), *Mombasa Swahili Women’s Wedding Songs: A Stylistic Analysis*, Tasnifu ya uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Wafula, M. na Njogu, K. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*: Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.
- Wamitila, K.W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Phoenix Publishers Limited, Nairobi.
- \_\_\_\_\_, (2003), *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.
- \_\_\_\_\_,(2003), *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Limited.
- \_\_\_\_\_,(2008), *Kanzi ya fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

## **KIAMBATISHO**

### **1. NYIMBO ZA HARUSI ZA KISWAHILI**

**Tupendane wabaya waulizane –Mzee Yusuf**

**Siku zote wa kuombwa ni Mungu  
Yetu sote alopanga ni Mungu  
Hawa maadui zetu wanafanya kila hila  
Na hili penzi letu linalindwa na Mola  
Hatuwapi nafasi tunaapa tuliendeshe  
Hawa wapambe nuksi jeuri tutawaonyesha  
Kutwa tunaomba Mungu tunaomba Mungu  
Wasije leta majungu  
Tunapendana kizunguzungu,kwa matamu na machungu  
Oh!mpenzi wangu,wabaya wetu macho wameyakondoa  
Oh! Tuzidi kuomba Mungu, penzi letu lizidi kuendelea**

**Honey, nataka unibebe unipeleke kuoga  
Sweetie unilishe nishibe hata mlo uso mboga  
Kisha unipe kila kitu tulichohalalishiwa  
Nami nikupe mavitu,we mwenyewe unanijua  
Kisha tuchaze sebende letu mpaka joto analia  
Kwa kila mmoja wetu wakituona tazimia.**

**Tupendane kwelikweli wabaya waulizane  
Unijali nikujali vipembeni wanong'one  
Amebani makatili penzi letu wasilione  
Liwaume penzi hili vipembeni wanong'one  
Liwaume penzi hili dawa wasizione**

**Unavyocheza sebende I love you darling  
Akikutaka ni bure I need you sweetly**

**Ah,ayuni wangu wapuuze hao**  
**Raha ya ulimwengu wapuuze roho**  
**Wababa wabaya walimwengu wakitaka lao lazima watimize**  
**Sweety usiku unibembeleze uje mwema usingizi**  
**Honey taratibu unilaze, tukutane Kwenye njozi**  
**Tuwaone wenyе vivu watapojitia kitanzi**  
**Wale wenyе roho mbovu watakonda kama uzi**  
**Ah!sisi tuko kwenye maloavu, tunafanya makamusi**  
**Tunakula tunda mbivu kwa manakishi na mapozi**

**Tupendane kwelikweli wabaya waulizane**  
**Unijali nikujali vipembeni wanong'one**  
**Amebani makatili penzi letu wasilione**  
**Liwaume penzi hili vipembeni wanong'one**  
**Liwaume penzi hili dawa wasizione**  
**Unavyocheza sebende I love you darling**  
**Ah! Itabiti wangu usipunguze dozi ,mimi bado sijapoa**  
**Daktari wangu dawa zako wewe ndo zitonisaidia**

**Ah!sweety asubuhi nikiwa hoi, wayaja na makamusi**  
**Honey basi nipe chai yenyе nyingi tangawizi**

**Tupendane kwelikweli wabaya waulizane**  
**Unijali nikujali vipembeni wanong'one**  
**Amebani makatili penzi letu wasilione**  
**Liwaume penzi hili dawa wasizione**  
**Unavyocheza sebende I love you daring**  
**Akitaka ni bure**  
**Tutoke tukatanue kokote katika nchi**  
**Kokote wewe nambia weisei cocobichi**  
**Kisha nitayarishie juizi ya parachichi**  
**Wazushi tuwaringie timu yetu kali kwa mechii**  
**Timu yetu kali kwa mechii**

**Wawili wakipendana adui hana na fasi  
Mbona mtaumwa sana ,nyiye wabaya wanafsi  
Nuru imetuakia tunamshukuru Mungu  
Wale walotupangia na kutuletea majungu  
Mungu atawaunga kwa miiba ya sungu  
Pendo tumelizingua kwa yasini tatu  
Lisije kuhusudiwa na macho ya watu**

## **2. HARUSI - ISSA MATONA**

**Hongera mwanangu eee x2  
Hongera mwanangu eee x2  
Sisi wazazi aseme yu wapi?  
Wapi mama Harusi  
(Aje hapa tuhangaike naye) x4**

**Mamaye harusi aje hapa  
Tuhangaike naye  
Shangazi lake harusi naye nataka aje hapa  
Tuhangaike naye  
Na bibi yake harusi naye nataka aje hapa  
Tuhangaike naye  
Na somo yake harusi naye nataka aje hapa  
Tuhangaike naye.**

**Yu wapi mama harusi aje hapa  
Tuhangaike naye  
Aje tunfunze mwali aache kujedheheks  
Akiitwa na mumewe wajibu kuitika  
Akiitwa ewe bibi aitike labeka  
Umrithie mumeo kwa kila analotaka  
Aje hapa tuhangaike naye x 4**

**Hodi! Hodi! Nimekuja na la kushauri  
Nimekuja na la kushauri**

**Msongee karibu wala msikae mbali**  
**Makungwi karibu kusanyikeni**  
**Mwali amekuja leo ungo tutazaliwa lezi**  
**Aje hapa tuhangaike naye x 2**

(Ijapokuwa na mwao sitaki mnitukane) x2  
Nawaita wazazi waje hapa tuonane  
Wanipe mkaja wa kuzipata  
Uinue uso juu mama wahisani wakuone  
Ana pokuja mumeo nyumbani  
Hujambo muulizane  
Umpokee mkoba mama yaliyo ndani usione  
Utahadhari na soga wasije wakakunyanganya  
Mama na salubeti wengine si wanaume  
Leo umempata wako mama  
Maharada wako wakome  
Waje hapa tuhangaike naye x4

**Leo ni leo x2**  
**(Mtauona mpambano kweli si uongo)x3**

Somoye bibi harusi hebu nitafutieni  
Na makungwi wake harusi wote waje hapa uwanjani  
Waje tumfunze mwali malezi ya kizamani  
Unapopelekwa kwako mama  
Umfika nyumbani  
Ukacheke na mumeo mama umpumbaze chumbani  
Wakaja na ndugu zake  
Mama wakaribishe nyumbani  
Wakaja mawifi zake mama uinuke kitandani  
Wakaja wakwezo uwaweke ukumbini  
Waje hapa tuhangaike naye x4

**Wakaja shemeji zako mama uwaweke barazani  
Wakaja mashoga zako sema nao dirishani  
Wakikuaga kwaheri waambie karibuni  
Ufunge mlango wako urejee kitandani  
Ukasikia hodi! mama ushungi uwe kichwani  
Wenda ikawa ni mumewe mama  
Usife moyo kama ndiyemumeo  
Aje hapa tuhangaike naye x4**

### **3. QASIDA ZA HARUSI (HAMISA OBEID)**

**Imeshawadia na imeshatimia**

**Harusi ya barakaaax2**

**Tushangilie harusi minnn sunaaaa  
Ni jambo la kheri fiiii uumaaa.**

**Harusi ni sunna njema minnn sunnaaa  
Kitendo cha watu fiiii uumaaax2**

**Ndoa kwetu ni halali minn sunnaaa  
Ni jambo jamili ii fiiii uumaaa**

**Bwana harusi na bibi harusi x2  
Nuru ya kheri iwashukie<sup>x2</sup>  
Kwa radhi za Mtume aa aa aa  
Waishi kufanya mema  
Na watoto wao mola awajalie ee ee  
Nuru ya kheri iwashukie  
Fahamu nzuri uwabarikie x2**

### **4. MISTER MAHMOUD**

**Helo,helo,helo -I love you mr.Mahmoud  
Helo,helo,helo -I love you mr.Mahmoud  
Usiku huwaza sana kukicha silali tena**

**I love you Mr.Mahmoud.**

**Nakushukuru mpenzi kwako kuipata jaha  
Kunipa mema makazi na maisha yenye raha  
Kunipa mema makazi na maisha yenye raha  
Kuijenga yangu enzi kwa pendo lenye furaha**

**I love you Mr.Mahmoud.**

**I love you Mr.Mahmoud.**

**Menidhibiti kikweli mpenzi menizuiya  
Umeitweka akili yangu imenipotea  
Umenitweka akilli yangu imepotea  
Sitoki sendi mahali kwako nimeshazoea**

**I love you Mr.Mahmoud.**

**I love you Mr.Mahmoud.**

**Kiwa na wewe yakini jengine siliwazi  
Kwa maneno ya imani unipayo ni mapenzi  
Kwa maneno ya imani unipayo ni mapenzi  
Hupiga moyo kite kateremsha pumzi**

**I love you Mr.Mahmoud.**

**I love you Mr.Mahmoud.**

**Kwa hakika ni mwalimu mwenye makini kufunza  
Hodari ulohitimu mambo yako miujiza  
Hodari ulohitimu mambo yako miujiza  
Huna usilofahamu kila mtezo wateza**

**I love you Mr.Mahmoud.**

**I love you Mr.Mahmoud**

## **5. USICHE**

**Usiche bwana harusi usiche  
Usiche bwana harusi usiche  
Usiche bwana harusi usiche  
Ukiona bahari utaogelea  
Usiche bwana harusi usiche  
Usiche bahari utaogelea uvuke  
Usiche bwana harusi usiche**

**Usiche bibi harusi usiche  
Usiche bibi harusi usiche  
Usiche bibi harusi usiche  
Bwana akitaka tafadhali mpe.**

**Usiche bwana harusi usiche  
Usiche bwana harusi usiche  
Usiche bwana harusi usiche  
Umetowa pesa kununua chako  
Usiche bwana harusi usiche**

## **6. KHERI ISHALLAH**

**Kheri Ishallah Ishallah  
Kheri Ishallah baraka tele**

**(Kwa bwana kharousi na bibi kharousi) x4  
Wakae hadi milele  
Kwa sheria za Kiislamu.  
Furaha zimewajaa maharusi wetu hawaaa**

**Nyoyo imewatulia radhi  
Mola awabariki awabariki**

**(kweli minaallha akheri ya kharousi)x4  
Kwa baraka za Mtume**

**Wazae mke na rasuly  
Maisha yako mazuri.**

**Wahifadhi ya Qahari mabaya yalokithiri  
Kheri minaallhaa kheri ya kharousi  
Kwa kweli wamependana  
Ndio maana wakaoana  
Kheri kheri kheri minaallhaa  
Kheri minaallhaa kheri minaallhaa**

**7. SALAAM BWANA KHAROUSI  
(QASWIDA YA HARUSI)**

**Salamu ya salamu bwana kharousi  
Na bibi harusi salamu**

**Kwa bwana kharousi aishi salama  
Na bibi arusi twawaombea mema  
Wameshatimiza jambo lenye maana  
Alilohusia Mtume hesima**

**Jambo la kuoa mola huridhia  
Fanyeni mupesi upate tujika  
Wacha wasiwasi warizikijuwa  
Ilahi kudusi ndio anatowa**

**Ewe ndugu yangu wasuburi nini?  
Jambo la kuowa utafanya nini?  
Dunia hadaa maisha kalili  
Nakupa nasaha hebu yafikiri  
(Mawada mawaaada ya makhurousi) x4**

**Na dua ya kheri tunnnnnnawaombea  
Mawada mawaaada ya makharousi  
Maisha mazuri tunawatakia**

**Mawada mawaada ya makharousi  
Rabii duwa zetu bwana  
Mawaada yao makharousi**

**Waishi vizuri na maisha mema  
Mawada mawaada yao makharousi**

### **8. HEKO! (AMRI ABEDI)**

**Heko ! Amri Abedi mwenye fadhili na utu  
Heko !akupe wadudi faraja na kila kitu  
Heko !ukidhi muradi usitawi kati yetu  
Ndoa aridhi mlinzi , ndoa ardhie binti.**

**Heko! Mapenzi yazidi, walie wivu wenzetu  
Heko !lako lisirudi, wal lisishike kutu  
Heko !kijana asadi, katika biladi zetu**

**Ndoa aridhi mlinzi , ndoa ardhie binti.  
Heko !mwenye jjitihadi ,huwa tegemeo letu  
Heko !halitasaidi , la ujane kuwa kwetu  
Heko si umaridadi, sisi si wanyama mwitu  
Ndoa aridhi mlinzi , ndoa ardhie binti.**

**Heko ! Ndiyo makusudi, kiumbe kutenda utu,  
Heko !huwa na zwadi , nskutuza mwanakwetu  
Hekohazina idadi zatoka kwa kila mtu,  
Ndoa aridhi mlinzi , ndoa ardhie binti.**

**Heko !mchezo ni sudi,sudi yenyewe ni yetu,  
Heko !chano kimebidi , kuchukuliwa na watu  
Heko !sisemi zaidi, chano hiki cha wenzetu,  
Ndoa aridhi mlinzi , ndoa ardhie binti**

## **(II). NYIMBO ZA HARUSI ZA KIMERU**

### **1.MBIRIRA MUTHONI**

**Mbirira muthoni ntigucereri**

**Ni mbotiki ngwikaira ibungo x2**

**Mpumite kuraja tigucereri**

**Mucii jwa muthoni ntigucereri x2**

**Ni kagwiua ghetu kwija kwi muthenya**

**Mbaraniria na muthoni**

**Ni mbotiki ngwikaira ibungo x2**

### **TAFSIRI**

**Waambie wazazi wa bibi harusi**

**Sikutarajia kuchelewa nilikuwa nashona vifungo**

**Kwenye nguo ya harusi.**

**Waambie wazazi wake bibi harusi**

**Sikutarajia kuchelewa lakini tumetoka mbali sana.**

**Tulitarajia kufika mapema sana**

**Kwa wazazi wa bibi harusi**

**Lakini tulichelewa tukivaa mavazi ya harusi**

**Mbirira ngina nthaka aarete rubunguro**

**Nyomba e mutana ikwona muruguri x2**

**Ii ui ikwona muruguri**

**Ii ui ikwona muruguri**

**Guti gia gukira rete rubunguro**

**Tutwire kuromba rete rubunguro**

**Maromba jagukinya rete rubunguro**

**Tukwona ii murugi rete rubunguro**

**Mukami wa iria rete rubunguro**  
**Chairman wa kanisa rete rubunguro**

**Nyomba ii muthaka**  
**Ikwona muruguuri**

**TAFSIRI**

**Mwambie mama mkwe alete ufunguo**  
**Nyumba ya mwanawе**  
**Imepata wa kufungua (mkaaji)**

**Ii ui imepata mkaaji x2**  
**Hakuna cha kuogopa**  
**Maombi yetu yamejibiwa**  
**Wa kukamua tumempata**  
**Kiongozi wa kanisa**

**Nyumba ya bwana harusi**  
**Imepata mwenyewe**

**2. KAANA NI KEEGA**  
**Ii ii uu kaana ni keega**  
**Gatuma nthiora kithioro**  
**Ii ii uu nikarombairwe.**

**Ii ii uu kaana ni keega**  
**Gatuma nthiora kithioro**  
**Ii ii uu nikamenyairwe**

**Ii ii mwana ni wa Ncurubi**  
**Ii ii kaana ni keega**  
**Gatuma nthiora kithiro**  
**Ii ii uu nikamenyairwe**

**Ithe ni wa Gichunge**  
**Ii ii uu kaana ni keega**  
**Gatuma nthiora kithioro**  
**Ii ii uu nikarombairwe**

**Ncurubi iretiire mwerine ireja na ‘mobile’**  
**Twaragie Amerika**  
**Ii ii uu kaana ni keega**  
**Gatuma nthiora kithioro**  
**Ii ii uu nikamenyairwe**

#### **TAFSIRI**

**Mtoto ni mzuri amenifanya nisafiri mbali**  
**Aombewe.**

**Mtoto ni mzuri amenifanya nisafiri mbali**  
**Achungwe vyema.**

**Mtoto ni wa rika la “Ncurubi”**  
**Mtoto ni mzuri amenifanya nisafiri mbali**  
**Aombewe.**

**Babake ni wa rika la “Gichuge”**  
**Mtoto ni mzuri amenifanya nisafiri mbali**  
**Achungwe vyema.**

**Rika la Ncurubi” lilienda mwezini**  
**Wikaja na rununu (simu ya mkono)Ndio tuweze kuwasiliana hadi**  
**Marekani**  
**Mtoto ni mzuri amenifanya nisafiri mbali**  
**Achugwe vyema.**

### **3.GARURA MITHIIRE**

**Kiongozi : Garura mithii.....**

**Wote: Ayia garura mithiire x2**

**Kiongozi : Ndiunga ya aari.....**

**Wote: Ayia Tigania nayo x2**

**Kiongozi : Cia ekuru.....**

**Wote: Ayia ni thaa ikumi x2**

**Kiongozi : Ng'ombe iri nja.....**

**Wote: Ayia nigwe Mukami x2**

**Kiongozi :mukuru iri nja.....**

**Wote: Ayia nigwe murugiri x2**

**Kiongozi : nguo ciawe.....**

**Wote: Ayia nigwe muuri x2**

**Kiongozi : Twana twaku.....**

**Wote: Ayia nigwe mumenyeri x2**

**Kiongozi : ngino nthaka.....**

**Wote: Ayia nigwe mumenyeri x2**

**Kiongozi : Ucuru bwao.....**

**Wote: Ayia nigwe mukii x2**

**Kiongozi : muda jwaku.....**

**Wote: Ayia nigwe muandi x2**

### **TAFSIRI**

**Kiongozi : Badilisha miene.....**

**Wote: Ayia badilisha mienendo x2**

**Kiongozi : Nyendo za wasicha.....**

**Wote: Ayia achana nazo x2**

**Kiongozi : za akina mama (kurudi nyumbani).....**

**Wote: Ni saa kumi kamili x2**

**Kiongozi : Ng'ombe aliye nyumbani.....**

**Wote: Ayia ndiwe wa kukamua x2**

**Kiongozi : Mmeo aliye humu.....**

**Wote: Ayia ndiwe wa kumpikia x2**

**Kiongozi : Nguo zake.....**

**Wote: Ayia ndiwe utakayefua}x2**

**Kiongozi : watoto wako.....**

**Wote: Ayia ndiwe utakayewachunga}x2**

**Kiongozi : mama mkwe.....**

**Wote: Ayia ndiwe utakayemchunga}x2**

**Kiongozi : uji wao.....**

**Wote: Ayia ndiye mtengenezaji x2**

**Kiongozi : Shamba lako.....**

**Wote: Ayia ndiwe utakayepanda x2**

#### **4. GIKUBWA KIATHO**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho x2**

**Muthenya i munene gikubwa ii ii**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho**

**Wona ngina nthaka umwitage ‘maami’**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa ii ii**

**Gikubwa kiatho x2**

**Ona ithe wa nthaka umwitage “baaba”**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho**

**Onagwe mugurani gikubwa ii ii**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho**

**Utiletiire kwa ba mwari gikubwa ii ii**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho**

**Kinya bo niaciari benu gikubwa ii ii**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho**

**Ukabagwatira nthoni gikubwa ii**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho**

**Ukamwitaga “ntii”umwitage “maami”**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho**

**Niwe wakua rwaku rwa njara**

**Ya kimotho (gikubwa ii ii x2)**

**Gikubwa kiatho**

**Na nguo cia muthaka nigwe ukauraga**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho**

**Ukimwitaga ‘munyanya’ gikubwa ii ii**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho**

**Wendo ni bunene ni rwaru rwaku**

**Gikubwa ii ii**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho**

**Ukwona murugi na mutwiri wa ng’ombe**

**Gikubwa ii ii**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho**

**Onagwe ngina nthaka ukanywa ‘obatini’**

**Ya ‘milo’gikubwa ii ii**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho**

**Urugiri ni muko mutana gikubwa ii ii**

**Gikubwa ii ii x2**

**Gikubwa kiatho**

**TAFSIRI**

**Harusi imefana sana x2**

**Siku imekuwa njema na harusi imefana sana**

**Kumekuwa na ushirikiano mzuri**

**Harusi imefana sana**

**Umwonapo mama mkwe umwite ‘mama’**

**Harusi imefana sana**

**Na wewe bwana harusi, harusi imefana**

**Harusi imefana sana.**

**Usikose kuwatembelea wakwezo harusi imefana**

**Harusi imefana sana.**

**Hata wao ni wazazi wenu,harusi imefana**

**Harusi imefana sana.**

**Unapaswa kuwahesimu,harusi imefana**

**Harusi imefana sana**

**Umwonapo mamamkwe umwite ‘mama’**

**Harusi imefana sana**

**Ndiye aliyekupa ubavu wako wa kushoto,**

**Harusi imefana sana**

**Nguo za mumeo ni wewe utafua,**

**Harusi imefana sana**

**Mumeo utamwita ‘mpenzi’ wako**

**Harusi imefana sana**

**Usimwaibishe kamwe,**

**Harusi imefana**

**Mpenzi ni makuu ni ubavu wako**

**Harusi imefana sana**

**Umempata mpishi na mfugaji wa ng’ombe**

**Harusi imefana sana**

**Hata wewe mama ,mkwe utapikiwa**  
**Chai ya milo, Harusi imefana sana**

## **5. MWANA TI MBETIRI**

**Kiongozi: Mwana ti mbetiri atuura ngariine**  
**Wote: Mwana ti mbetiri atuura ngarine x2**

**Kiongozi: Mwana ti ncaabi araara gwakirua**  
**Wote: Mwana ti ncaabi araara gwakirua x2**

**Kiongozi: Mwana ti mwere atindua maegone**  
**Wote: Mwana ti mwere atindua magonex2**

**Kiongozi: Guti gia gukira ii ui**  
**Murungu ari mbere ui**  
**Niatukaritie atindwa ngarine**  
**Wote : mwana ti mwere atindua maegone**

**Kiongozi: Tutwire kuromba akabwa ma maego**  
**Wote: Mwana ti ncaabi araara gwakirua**

**Kiongozi: Mwana ti ikwachii atumwa na neti**  
**Wote: Mwana ti ikwachii atumwa na neti**

**Kiongozi : Murungu arokumwa ui**  
**Acore betu ii ui**  
**Tutwire kuromba atumwa na neti**  
**Wote: Mwana ti ikwachii atumwa na neti**

## **TAFSIRI**

**Kiongozi : Mtoto sio betri aishi kwa gari**  
**Wote : Mtoto sio betri aishi kwa gari x2**

**Kiongozi : Mtoto sio maharagwe apikwe usiku kucha**

**Wote : Mtoto sio maharagwe apikwe usiku kucha**

**Kiongozi : Mtoto sio mawele ashinde kwenye kinyua**

**Wote : Mtoto sio mawele ashinde kwenye kinyua**

**Kiongozi : Hakuna la kuogopa kwani**

**Mungu yuko mbele yetu anatuongoza**

**Wote : Mtoto sio betri aishi kwa gari**

**Kiongozi: Tumeomba kwa muda mrefu**

**Mtoto sio betri aishi kwa gari**

**Kiongozi : Mtoto sio gunia la viazi**

**Ashonelewe neti hapo juu**

**Wote : Mtoto sio betri aishi kwa gari**

**Kiongozi : Sifa kwa mungu tumeishi kuomba**

**Wote : Mtoto sio betri aishi kwa gari.**

## **6.MWANA II MUTUNDA**

**Mwana ii mutunda**

**Mutunda ii kajurimairwa**

**Ciorwa cioimaku**

**Mwana ii mutunda**

**Mutunda ii kajurimairwa**

**Ciuma Nthimbiri**

**Mwana ii mutunda**

**Mutunda ii kajurimairua**

**Mwana ni wa uguri bubumu**

**Mwana ii mutunda**

**Mutunda ii kajurimairua**

**Mwana ni wa goro**  
**Mwana ii mutunda**  
**Mutunda ii kajurimairua**

**TAFSIRI**

**Mtoto ni mti (wa mtunda)**  
**Mtunda unapaliliwa x2**

**Mtoto ametoka wapi?**  
**Mtoto ni mtunda**  
**Mtunda ii unapaliliwa**

**Ametoka Nthimbiri**  
**Mtoto ni mtunda**  
**Mtunda ii unapaliliwa**

**Mtoto ni ghari**  
**Mtoto ni mtunda**  
**Mtunda ii unapaliliwa.**

**7. KINANDA IGIKUCHWE**

**Irii riri nandi iri riri nandi**  
**Irii riri nandi iri riri nandi**

**Kinanda igikuchwe**  
**Kienda gutwika igitwike**  
**Irii riri nandi**  
**Muthaka agure kingi**  
**Iriri riri nandi**  
**Twinire muiki**  
**Iriri riri nandi**

**Muiki wina neti**  
**Iriri riri nandi**  
**Iriri riri nandi Iriri riri nandi**

**Kinanda igikuchwe**  
**Gikuchirwe mugongo**  
**Iriri riri nandi**  
**Gikuchirwe bwe iguru**  
**Iriri riri nandi**  
**Kienda gitwi igitwike**  
**Iriri riri nandi**  
**Muthaka agure kingi**

**Iriri riri nandi Iriri riri nandi**  
**Muiki turi nawe ii ii riri nandi**  
**Murungu aromwa ii Iriri riri nandi**  
**Mpongeri mwirigene ii Iriri riri nandi**  
**Kinanda igikuchue ii Iriri riri nandi**  
**Igikuchue gia kauna**  
**Iriri riri nandi**

**TAFSIRI**  
**Leo ni leo**  
**Kinanda kichezwe**  
**Nyaya zikikatika bwana harusi atanunua**

**Tuchezee bibi harusi**  
**Bi harusi aliyefunikwa net**  
**Leo ni leo**  
**Kinanda kichezwe**  
**Kichezewe juu**  
**Kichezewe mgongoni**  
**Kikikatika bwana harusi atanunua kingine**

**Leo ni leo  
Bibi harusi tunaye  
Mungu asifiwe  
Ongezeko la mtu kijiji  
Kinanda kichezewe  
Kichezewe mgongoni.**